epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Mei 8, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581670
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital


Jumatano Mei 8, 2024 Nipashe 9

HOTUBA YA WIZARA YA ELIMU

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MUHTASARI WA HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF F. MKENDA (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025

Prof. Adolf Faustine Mkenda
Waziri

OS. Omari Juma Kipanga
Naibu Waziri

Dkt. Franklin Jason Rwezimula
Naibu Katibu Mkuu

Prof. Carolyne Ignatius Nombo
Katibu Mkuu


Prof. James Epiphan Mdoe
Naibu Katibu Mkuu

UKURASA 9

## MUHTASARI WA HOTUBA YA BAJETI YA WIZARA YA ELIMU

# Vipaumbele vitano vya elimu 2024/25

UKURASA 2




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

UKURASA WA 4

**Samia** atoa maagizo mapya athari kimbunga Hidaya



UKURASA WA 7

**Bil.** 11/- zalipwa kifuta machozi kwa waathirika wa wanyamapori



UKURASA WA 17

**Vyama** vyakosoa kebehi za Tundu Lissu



## Rais Dk. Mwinyi akaribisha uwekezaji maji, umeme

UKURASA 3



Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni

# TAKUKURU yatoa kauli uchunguzi madai ya fedha chafu CHADEMA

UKURASA 8

MICHEZO MGUNDA: MECHI NA AZAM NI KAMA FAINALI UK.24 KATUNI UK.6



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (kushoto), akijadiliana jambo na Naibu wake, Ridhiwani Kikwete, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vipaumbele vitano sekta ya elimu 2024/25

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeanika vipaumbele vikuu vitano kwa 2024/25 vinavyolenga kuleta mageuzi katika sekta ya elimu, kikiwamo ujenzi wa shule mpya 100 za sekondari za ufundi ambazo 26 kati ya hizo, zitaanza kupokea wanafunzi kuanzia Januari, mwakani.

Pia imesema serikali itaongeza fursa za utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wenye sifa na uhitaji kutoka 223,201 hadi 252,245 na wanafunzi 84,500 wa mwaka wa kwanza watanufaika. Pia wamo wa shahada ya kwanza 80,000, shahada za juu 2,000, wanaosoma nje ya nchi 500 na Mfuko wa Ufadhili ya Samia (Samia Scholarship) 2,000 na wanafunzi 157,745 wanaoendelea na masomo.

Akiwasilisha jana bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka 2024/25, Waziri Prof. Adolf Mkenda aliomba Bunge kupitisha Sh. trilioni 1.96 ili kutekeleza vipaumbele hivyo, vinavyolenga kuimarisha ubora wa elimu ili vijana wapate maarifa, ujuzi, kujiamini, kujiajiri na kuajirika.

Prof. Mkenda alitaja vipaumbele vingine kuwa ni kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria na kuandaa miongozo ya utoaji elimu na mafunzo nchini na pia kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (amali na amali sanifu), kuimarisha ubora wa elimu ya msingi, sekondari na ualimu.

"Kipaumbele kingione ni kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu na kuendeleza utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu," alisema.

**MABORESHO MITAALA**

Alisema kwa mwaka ujao, serikali itafanya mapitio ya mitaala 171, kuandaa mitaala mipya 18, kuanzisha programu za vipaumbele 145 na matumizi ya mbinu bunifu za ufundishaji katika elimu ya juu.

Serikali, alisema itaanzisha vituo vya elimu huria (OER) ili kuimarisha majukwaa ya ndani na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya juu; itasasisha na kuandaa mtaala mpya katika taasisi 17 za elimu ya juu na itahakiki mitaala 230 ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

"Lengo ni kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanakidhi mipango ya nchi, soko la ajira la kitaifa na kimataifa na kuwawezesha wahitimu kujiajiri na kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira," alisema.

"Serikali pia itaandaa mwongozo wa elimu jumuishi wa ufundishaji na matumizi ya teknolojia kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji na matumizi ya teknolojia katika elimu na mafunzo; itafanya mapitio ya mwongozo wa uanzishaji na usajili wa shule wa mwaka 2020 ili kuendana na mabadiliko ya sera na mitaala," alisisitiza.

kadhalika, alisema itakamilisha mwongozo wa kuwatambua na kuwaendeleza wanafunzi wenye vipawa na vipaji; itaandaa kiunzi, mwongozo na zana kwa ajili ya kuwezesha upimaji wa ujifunzaji kwa wanafunzi katika ngazi husika.

**UFUNDI NA UFUNDI STADI**

Alisema ujenzi wa shule hizo mpya za amali (ufundi na ufundi stadi) utapewa kipaumbele katika maeneo ambayo hayana vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi au shule ya amali ya sekondari.

"Serikali itasajili vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi 150 ambapo vyuo vya elimu ya ufundi ni 100 na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 50, hivyo kuwa na jumla ya vyuo 504 vya elimu ya ufundi na vyuo 885 vya mafunzo ya ufundi stadi," alisema.

Alisema usajili wa taasisi hizo utawezesha kuongeza fursa na kutoa mafunzo kwa kuzingatia viwango na ubora.

Alibainisha kuwa wanafunzi 263,718 watadahiliwa wa elimu ya ufundi na mafunzo na ufundi stadi kati yao wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi ni 190,518 na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 73,200 sawa na ongezeko la asilimia 23 ikilinganishwa na udahili wa mwaka 2023/24.

Alisema udahili unalenga kuongeza rasilimaliwatu yenye ujuzi na uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa.

## Bodi ya Mikopo kupewa 'meno' zaidi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema kwa mwaka 2024/25 itafanya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ili kuongeza ufanisi wake ikiwamo kurahisisha ufunguaji wa mashauri na utekelezaji wake.

Akiwasilisha bungeni jana makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka huo, Waziri Prof. Adolf Mkenda alisema wataendelea kukusanya madeni ya mikopo iliyoiva ya kiasi cha Sh. bilioni 198 kutoka sekta ya umma na kuimarisha makusanyo kutoka sekta binafsi na isiyo rasmi.

Aidha, alisema itatafuta wanufaika wapya 40,000 wenye marejesho ya mikopo iliyoiva ikijumuisha wanufaika wapya 5,000 wenye mikopo chechefu kutoka sekta binafsi na isiyo rasmi.

Pia alisema ufadhili kwa ajili ya shahada za juu ikiwamo eneo la fani ya mionzi na nyuklia utaanza kutolewa na itafanya tathmini ya programu 300 za masomo mbalimbali katika vyuo vikuu nchini.

MIKOPO DIPLOMA

Pia alisema serikali itatoa mikopo kwa wanafunzi wa stashahada takribani 10,000 katika fani za kipaumbele na zenye uhaba wa wataalam nchini, zikiwamo za sayansi na ufundi.

Alisema ili kuimarisha ushirikiano na mataifa mengine na kuongeza fursa za elimu nchini, serikali itatoa ufadhili kwa wanafunzi watano kutoka China wanaosoma lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

Pia itatoa ufadhili kwa wanafunzi watano raia wa Oman na wanafunzi watano raia wa Hungary kusoma katika vyuo vikuu nchini kulingana na mikataba na itashiriki katika mikutano ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Alisema serikali itaandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu na kwamba itafanya utafiti wa kimkakati wa ulinganishaji katika nchi ambazo vyuo vikuu vina uzoefu wa kutumia teknolojia ya kidijiti katika ufundishaji na ujifunzaji na huduma za utawala.

Katika kuimarisha matumizi salama ya mionzi ya nyuklia nchini, Prof. Mkende alisema alisema serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki itaendelea kudhibiti matumizi ya mionzi nchini kwa kukagua vituo 900 ikiwamo hospitali, vituo vya afya, migodi, viwanja vya ndege, na viwanda na majengo yenye mashine za kupima mionzi ili kuhakikisha uwepo wa mazingira salama kwa wagonjwa, wafanyakazi na umma kwa ujumla.

HABARI KITAIFA

# Wawili mbaroni madai kuuza mlima wa serikali

Na Beatrice Shayo

WATU wawili, akiwamo Mwenyekiti wa Kitongoji cha Msowero A, Petro Sanga (Paroko), wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuuza eneo la mlima, mali ya kijiji cha Msowero, Kilosa mkoani Morogoro kwa Sh. milioni 20.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka, aliagiza kukamatwa kwa mwenyekiti huyo na mwenzake Awadh Ngajime.

Shaka alitoa amri hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa hadhara alipokuwa akisikiliza kero za wananchi wa Kata ya Msoweto A.

Alisema watu wengine 48 ambao wanaosadikiwa kuwa sehemu ya mtandao uliohusika kuuza mlima huo kinyume cha utaratibu wenye jumla ya ekari 1,158 wanaendelea kutafutwa.

Shaka alisema kumekuwa na wimbi la uvamizi wa maeneo ya ardhi unaoonekana kukithiri siku hadi siku na baadhi ya maeneo wananchi wamekuwa wakihusika kuyauza kinyume cha sheria.

"Tuna kata saba ndani ya wilaya hii zinaongoza kwa migogoro ya ardhi ikiwamo hii ya Msowero, mnaongoza mnavamia maeneo ya serikali. Viongozi wapo mnashirikiana nao kisha mnageuka, mnasingizia viongozi wa wilaya, mkoa na taifa kuwa wanakuja kupora ardhi yenu kumbe ni uongo," alisema.

"Mmeuza mlima kinyume na utaratibu ekari 1,158 zote mmevamia na kuuza. Hii ni mali ya serikali ya kijiji kisha mnageuka kushutumu wengine kumbe ninyi wenyewe ndio wahusika. OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) huyo mwenyekiti aliyeshiriki kuratibu mauziano na kulipwa Sh. 500,000 na huyu aliuza eneo la mlima kwa Sh. milioni 20 naondoka nao. Pia naagiza watu wengine 48 waliohusika kwenye kuuza wajisalimishe polisi, vinginevyo watafutwe popote walipo na wafikishwa kwenye vyombo vya sheria," alisisitiza.

Aidha, Shaka alipiga marufuku na kuweka zuwio la kuendeleza shughuli yoyote katika eneo la mlima unaodaiwa kuuzwa, huku akisisitiza kuwa walioziwa maeneo hayo wametapeliwa na bado ni mali ya serikali.

"Viongozi mpo mnayaona kitongoji, kijiji, kata wote mnajua lakini mnalea uovu huu, haiwezekani kila aliyehusika kwenye hili hatabaki salama ili iwe fundisho kwa wengine, naomba wajulisheni wote walionunua eneo lile wametapeliwa na hatutasita kuchukua hatua kwa yoyote atakaekaidi maelekezo ya serikali," alisema.

Shaka alisema ameshangazwa na viongozi wa chama kimoja cha siasa wakilibeba jambo hilo wakidai wananchi wananyanganywa ardhi wanapigwa na kuondolewa katika maeneo yao.

"Kumbe mmewalisha matango pori mnaficha uovu wenu na wao kwa kwa vile maarifa yao madogo wakaona ndio ajenda ya kuibeba limebuma sasa warudi kukanusha uongo waliouanisha umma wa Watanzania," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Msowero, Abdalla Machera, alimweleza Shaka kuwa katika siku za karibuni, viongozi wa kisiasa wamekuwa wakifika katika maeneo yao, huku wakilazimisha wananchi kupigwa picha na kutoa malalamiko au shutuma za uongo kuhusiana na serikali jambo ambalo sio la kiungwana na kistarabu.

"Mheshimiwa DC unayoyasikia huko ni kutaka kuchafua kata yetu na viongozi wetu ili wao kutafuta kuungwa mkono kwa mambo ya uongo na uzushi. Yaliopo hapa ni baadhi ya wananchi kujihusisha katika matendo maovu, sasa wakiona mnataka kuwachukulia hatua, wanakimbilia kwa viongozi wa kisiasa ili wapaze sauti wakidhania wanaweza kuzima uovu wao wasichukuliwe hatua kwa makosa yao. Haiwezekani wameuza mlima wetu ekari 1,158," alisema.

# Rais Mwinyi akaribisha uwekezaji maji, umeme

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inahitaji uwekezaji mkubwa wa sekta za maji na umeme ili kuongeza ufanisi wa huduma katika maeneo hayo.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo jana alipozungumza na uongozi wa Kampuni ya WAPCOS ya nchini India, uliofika Ikulu visiwani humo.

Dk. Mwinyi alisema hadi sasa Zanzibar inapokea megawati 110 za umeme, ambazo pia inapata msaada kutoka Tanzania Bara na kwamba serikali ina dhamira ya kuzalisha umeme wake na iko tayari kushirikiana na kampuni yoyote itakayokuwa tayari ili kuanza hatua za upembuzi yakinifu.

Rais Dk. Mwinyi pia alisema Zanzibar inahitaji utafiti wa kina wa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme kwa kuangalia zaidi uwekezaji na huduma za uhakika.

Dk. Mwinyi aliikaribisha kampuni ya WAPCOS endapo inavutiwa kufanya kazi na serikali ya Zanzibar.

Alisema serikali za Zanzibar na India ni wadau wakubwa kwenye huduma za jamii na zinashirikiana kwenye nyanja mbalimbali za maendeleo, ikiwamo elimu.

Naye Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa WAPCOS, Rajni Kant Agrawal, alisema kampuni yao imejikita zaidi na kutoa huduma za ushauri hasa kwenye nishati ya umeme, maji na miundombinu na kwamba iko tayari kushirikiana na serikali kwenye uwekezaji wa sekta hizo.

Alisema kwa Tanzania tayari kampuni hiyo inafanya kazi maeneo ya Dar es Salaam, Bagamoyo na mengine ya nchi, ikiwamo Zanzibar.

Kampuni ya WAPCOS Limited yenye makao makuu yake New Delhi, India ni watoa huduma za ushauri kwa nyanja za rasilimali maji, nishati na miundombinu. Ilizinduliwa rasmi Juni 26, 1969, New Delhi.

Ni kampuni yenye miradi kadhaa nchini humo, Asia na Afrika, iko chini ya umiliki wa serikali ya India kwa usimamizi wa Wizara ya Jal Shakti.




Vigezo na Masharti Kuzingatiwa

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Samia atoa maagizo mapya athari za kimbunga Hidaya

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Rais Samia Suluhu Hassan akitoa maelekezo ya huduma za dharura kupelekwa maeneo yaliyoathiriwa na kimbunga Hidaya, hatua zimeanza kuchukuliwa ikiwamo kurejesha mawasiliano ya barabara ya Lindi-Mtwara na kuwapa misaada waathirika.

Maeneo hayo ni pamoja na Mafia mkoani Pwani, Kilwa mkoani Lindi na Ifakara mkoani Morogoro, ambayo yameathiriwa na kimbunga hicho baada ya kuripotiwa kuwapo nchini mwishoni mwa wiki iliyopita.

Katika kikao cha dharura cha Kamati ya Maafa Kitaifa ambacho Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alikiitisha juzi ili kupokea taarifa ya hatua zilizochukuliwa kwenye maeneo hayo, alisema Rais Samia ameelekeza huduma za dharura zipelekwe mara moja.

Majaliwa alisema Rais Samia ameelekeza kuchukuliwa hatua za haraka katika maeneo yote yaliyoathiriwa na mvua zilizotokana na athari za kimbunga hicho ikiwa ni pamoja na kupeleka misaada.

Aidha, alisema Rais ameagiza Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lihakikishe linakamilisha uokoaji katika maeneo ya Kilwa na zaidi ya kaya 40 zimezingirwa na maji.

"Jeshi la Zimamoto mmefanya kazi kubwa, hakikisheni maeneo yenye makazi yaliyozingirwa na maji, wakazi wake wanaondolewa na kupelekwa maeneo salama pamoja na kupewa huduma zote muhimu," aliagiza.

Majaliwa aliagiza Wizara za Ujenzi, Uchukuzi, Afya, Maji, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mambo ya Ndani ya Nchi, Ulinzi na Fedha zichukue hatua za dharura ili kuhakikisha hakuna madhara zaidi yanayotokea katika maeneo yaliyopatwa na athari.

"Wizara ya Ujenzi endeleeni kuchukua hatua zote za dharura zinazohitajika kuhakikisha maeneo ya barabara yaliyokatika yanarekebishwa na huduma za usafiri zinarudi haraka," aliagiza.

Alipongeza jitihada zinazofanywa na idara ya menejimenti ya maafa kwa kuendelea kufanya uratibu katika maeneo yote yaliyoathirika na kuwataka waendelee na uratibu katika maeneo yaliyopata madhara kuanzia juzi.

"Ongezeni nguvu katika maeneo ya Ifakara, Kilwa na Mafia na kuhakikisha wananchi wote walioathiriwa wanakuwa salama na wanapata huduma zote za msingi za kijamii," aliagiza Majaliwa.

Waziri Mkuu pia, aliiagiza Kamati ya Maafa ya Kitaifa izisimamie kamati za mikoa na wilaya ili misaada inayotolewa kwa waathirika iwafikie walengwa.

**BARARARA LINDI-MTWARA**

Akizungumza wakati akiwa Nangurukuru wilayani Kilwa, Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema hadi kufikia leo au kesho barabara ya Lindi-Dar es Salaam itaanza kupitika, kutokana na serikali kutoa fedha za dharura kwa ajili ya kurejesha mawasiliano.

Mawasiliano ya barabara hiyo yalikatika tangu Jumapili na hivyo kusababisha abiria waliokuwa wakisafiri kuelekea mikoa ya Lindi, Mtwara na Dar es Salaam kukwama.



"Niendelee kuwatoa hofu wananchi na wasafiri wanaotumia barabara hii inayounganisha mikoa ya kusini, tangu jana (juzi) nimepiga kambi huku, nilianzia Somanga na sasa hivi tupo upande huu wa Nangurukuru, kama mnavyoona pande zote wanaendelea na kazi, bado tunaamini ndani ya saa 72, kufikia Alhamisi tutakuwa tumekamilisha kazi ya kurudisha mawasiliano ya barabara hii," alisema Bashungwa.

Alimwagiza Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mohamed Besta, kuongeza idadi ya malori yanayosomba mawe pamoja na mitambo inayotumika kupakia mawe hayo katika magari, ili kuongeza kasi ya kujaza vifusi katika eneo la barabara yaliyosombwa na maji.

Bashungwa alisema kuwa pamoja na jitihada za kuagiza makalvati ya plastiki yanayotumika katika dharura za kurejesha mawasiliano ya barabara kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo kwa wakati, lakini watalazimika kutumia makontena kwa kuyakata yatumike kama mbadala wa kalavati na kuwezesha maji kupita.

"Tunahitaji mawe ya kutosha ya kujaza katika eneo la mita nne na la mita 100 na kuweka makaravati, niwahakikishie kwamba kazi hii tunaimaliza ndani ya saa 72 kama tulivyosema kwa kuwa kila kitu tumepata, vifaa tunavyo, mitambo ipo."

Eneo la barabara lililoharibika ni la mita 80 katika barabara ya Somanga-Mtama na pia tuta la barabara hiyo limekatika katika eneo la Mikereng'ende umbali wa kilomita 10 kutoka Somanga uelekeo wa Lindi.

Pia katika Lingaula barabara imekatika kwa umbali wa kilomita 12 kutokea Nangurukuru uelekeo wa Lindi.

Uharibifu wa barabara hiyo ulisababishwa na mvua kubwa zilizonyesha mwishoni mwa wiki mkoani humo zilizoambatana na upepo mkali.

**WAATHIRIKA WAKUMBUKWA**

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Kanda ya Kusini imekabidhi bati zaidi ya 100 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 2.7 kwa ajili ya waathirika wa mvua na upepo zaidi ya 300 kutoka vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Masasi ambao nyumba zao zimeezuliwa na kubomoka hivyo kukosa makazi ya kuishi hadi sasa.

Msaada huo umetolewa jana mjini Masasi na kukabidhiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa, Wilaya ya Masasi ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Loutery Kanoni ili aweze kwenda kuwakabidhi waathirika hao.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo wa kukabilishi wa Taasisi ya TFS Wilaya ya Masasi, Mhifadhi Misitu Kanda ya Kusini, Anderson Besisila, alisema kutokana na wakazi zaidi ya 300 katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo kuathiriwa na mvua na upepo na kubomoa nyumba zao FTS kama wadau wameamua kutoa msaada huo wa bati zaidi ya 100 kwa ajili ya waathirika hao.

Besisila alieleza kwamba TFS imeguswa na jambo hilo na kuona kuna umuhimu wa kutoa msaada huo wa bati 100 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 2.7 ili kuhakikisha waathirika hao wanarejea katika makazi yao.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Loutery Kanoni, alisema kuwa anaishukuru TFS kwa kutoa msaada huo wa bati zaidi ya 100.

Alisema katika Wilaya ya Masasi kuna zaidi ya waathirika 300 ambao wamepoteza makazi yao ya kuishi kwa kubomoka kufuatia mvua na upepo vilivyojitokeza wilayani hapa.

Kanoni alisema kuwa kufuatia athari hizo serikali wilayani Masasi iliomba msaada wa kuwasaidia waathirika hao ili kuweza kuwafariji na kwamba mwitio umekuwa chanya ambapo wadau mbalimbali wameshatoa misaada kama hiyo.

**KIMBUNGA HIDAYA**

Mei Mosi, mwaka huu TMA ilitahadharisha kuwapo kwa kimbunga hicho kutokea siku iliyofuata katika Bahari ya Hindi, kutokana na mkandamizo mdogo wa hewa Mashariki mwa Pwani ya Mkoa wa Mtwara.

Kwa mujibu wa TMA, mkandamizo huo mdogo wa hewa ulionekana kusogea kuelekea Pwani ya Tanzania na kuwapo kwake mpaka juzi (Mei 6).

Kutokana na kuwapo kwake, mvua kubwa iliyoambatana na upepo ilinyesha Mkoa wa Lindi na Mtwara na miongoni mwa athari ni pamoja zaidi ya madaraja manne wilayani Kilwa, barabara iendayo Dar es Salaam, yamesombwa.

Baadhi ya vijijini vimezungukwa na maji katika kata za Masoko, Mto Matandu, Songasi, Mitole, Likwatu, Mavuji na Machakama na zaidi ya watu 70 wako hatarini.

Athari nyingine ilijitokeza kwa vyombo vya usafiri baharini ambapo Jumamosi baadhi vilisimama kutoa huduma kwa siku moja baada ya kuwapo kwa upepo mkali.

Siku tatu zilizopita, mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa ilionyesha kuwa katika kipindi cha saa sita zilizopita, Kimbunga Hidaya kilipoteza kabisa nguvu yake baada ya kuingia nchi kavu katika kisiwa cha Mafia.

Mabaki ya mawingu ya mvua yaliyokuwa yakiambatana na kimbunga hicho yalisambaa katika maeneo mbalimbali ya ukanda wa Kusini mwa nchi husasan katika maeneo ya mikoa ya Lindi, Mtwara, Morogoro na maeneo jirani.

**Imeandikwa na Romana Mallya na Elizabeth Zaya (DAR) na Hamisi Nasri, MASASI**

## Kamati yaundwa kukusanya mapendekezo nyongeza kikokotoo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa serikali imeunda kamati ya kukusanya na kuchambua maoni na mapendekezo ya viwango vya nyongeza ya pensheni kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina ili kuwezesha maandalizi ya rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Taska Mbogo.

Mbunge huyo alitaka kujua ni lini serikali itawaongezea pensheni wastaafu wanaolipwa Sh. 100,000 kwa mwezi na Hazina.

Dk. Nchemba alisema kazi ya uchambuzi wa maoni na mapendekezo ya wadau kuhusu viwango vya nyongeza ya pensheni kwa wastaafu hao inatarajiwa kukamilika kabla ya Juni 30, mwaka huu.

Aidha, mbunge huyo alisema kumekuwa na malalamiko ya kanuni za ukokotoaji pensheni kwa wastaafu na kuhoji nini mkakati wa serikali kufanya mapitio ya kanuni hiyo ili iweze kuwasaidia wastaafu.

Aidha, alihoji mpango wa serikali wa kuwapa mafunzo wastaafu wanaolipwa pensheni na Hazina kabla hawajastaafu ili iweze kuwasaidia.

Akijibu maswali hayo, Dk. Nchemba alisema ili kufanyia kazi kanuni za ukokotoaji mafao, tayari kamati imeundwa inayohusisha sekta mbalimbali na wizara inayosimamia masuala ya utumishi inaendelea na zoezi kubwa ambalo linahusisha suala la pensheni kwa upana wake.

Kuhusu mafunzo, alisema wamepokea hoja hiyo licha ya kuwapo utaratibu huo na kwamba wataboresha kadiri ilivyoshauriwa.

**Dk. Nchemba alisema kazi ya uchambuzi wa maoni na mapendekezo ya wadau kuhusu viwango vya nyongeza ya pensheni kwa wastaafu hao inatarajiwa kukamilika kabla ya Juni 30, mwaka huu.**

# Majaliwa awafunda ma-RC utashi kisiasa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaagiza wakuu wa mikoa nchini kufanyakazi kwa kufuata utashi wa kisiasa wa Rais Samia Suluhu Hassan ambayo ni kutaka utekelezaji wa mapendekezo yote ya Tume ya Haki Jinai.

Alisema wakati akifungua warsha ya wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa ya kuwajengea uelewa kuhusu maboresho kwenye mfumo wa haki jinai na utoaji wa haki nchini yanayoendelea jijini Dodoma.

"Utashi wa kisiasa wa Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha mfumo wa utoaji wa haki jinai lazima udhihirike kwenu ninyi viongozi mlio karibu na wananchi. Hata hivyo, utashi huo hauwezi kudhihirika kwenu iwapo hamtakuwa na nia ya dhati ya kubadilika na kisha kuongoza mabadiliko kwenye maeneo mnayomwakilisha Rais wetu na hususan katika kuhudumia wananchi," alisema.

Aidha, alisema lazima viongozi na watendaji wa serikali wawe na uelewa wa kutosha ili wayasimamie na kutekeleza mapendekezo hayo muhimu kwa ustawi wa jamii yetu.

Alisema malalamiko ya wananchi katika masuala kadhaa ndiyo yaliyoweka msukumo kwa Rais kuunda Tume ya Haki Jinai na kuyakubali mapendekezo yaliyotolewa na hatimaye kuigeuza kuwa kamati ya kuandaa mikakati utekelezaji wa mapendekezo yake.

Aidha, alitaja mambo yanayolalamikiwa na wananchi ni sheria ndogo kwenye serikali za mitaa ambazo zinakinzana na sheria mama.

Mengine ni migogoro ya ardhi, matumizi mabaya ya madaraka ya ukamataji na desturi kwa wakuu wa mikoa na wilaya kuambatana na wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama katika ziara mbalimbali hata zile zisizohitaji vyombo hivyo, hali inayosababisha hofu kwa wananchi na kuwafanya washindwe kufikisha mawazo na kero zao kwa viongozi hao. Aidha, aliwataka viongozi wote walioshiriki warsha hiyo wazingatie maelezo yatakayotolewa ili kila mmoja awe chachu ya mabadiliko ya kifikra, kimtizamo na kiutendaji katika eneo lake.

Aliwataka wazingatie kuwapo majengo na miundombinu muhimu kwa ajili ya taasisi za Haki Jinai katika maeneo mapya ya utawala (wilaya) yaliyoanzishwa.

Awali, Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, alisema ofisi hiyo itasimamia utekelezaji wa maagizo na maelekezo yatakayotolewa katika warsha hiyo ili dhamira ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuona wananchi wanapata haki zao inafikiwa.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Othman Chande, alisema tume hiyo ilipokea mapendekezo 333 ya maboresho ya utendaji kazi wa taasisi za haki jinai katika maeneo mbalimbali.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa matukio ya uhalifu nchini yanazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka na juhudi kubwa zinaelekezwa kupambana na uhalifu badala ya kubaini na kuuzuia.

# Polisi Singida yakamata 235

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JESHI la Polisi mkoani Singida limewakamata watu 235 kwa tuhuma za makosa mbalimbali ya jinai, zikiwamo ubakaji na ulawiti wakati wa msako wa kutanzua na kuzuia uhalifu unaoendelea mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Amon Kakwale, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema watuhumiwa hao walikamatwa katika kipindi cha Februari hadi Aprili, mwaka huu.

Alisema kuwa watu hao 135 walikamatwa wakiwa na bangi zenye uzito wa kilo 172 na wengine 46 walikutwa na mirungi na watano walikutwa na dawa za kulevya aina ya heroine zenye uzito wa gramu 0.82.

Kamanda Kakwale alisema watuhumiwa wengine 11 walikamatwa wakiwa na pombe ya moshi (gongo) lita 123, watatu wakiwa na ndoo 31 za mafuta ya kupikia aina ya safi mali ya Kampuni ya Mohamed Enterprises Limited zenye ujazo wa lita 20 kila moja.

Watuhumiwa wengine watano walikamatwa na televisheni 'flat screen' sita.

Kamanda Kakwale aliongeza kuwa katika misako na doria hizo walikamata watuhumiwa watatu wanaojihusisha na hujuma katika miundombinu ya umeme wakiwa na transformation 159KVA namba TX006524 aina ya TCO yenye thamani ya Sh. milioni 7.5 pamoja na nyaya za shaba.

Aliongeza watuhumiwa wengine watatu walikamatwa wakiwa na miundombinu ya umeme ya Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO) vipande 63 vya Polymeric Post Insulators ambavyo walivifunga kwenye viroba nane tayari kwa ajili ya kuvisafirisha kwenda kuviuza mkoani Singida.

Kamanda Kakwale alisema watuhumiwa wengine wawili walikamatwa wakiwa na betri saba za minara ya simu aina ya North Star zenye uwezo wa N-170 mali ya kampuni ya Helois Tower Tanzania na wengine wanne walikamatwa kwa kosa la kukutwa na jenereta lenye uzito wa tani moja mali ya kampuni ya minara ya simu ya Noven. Aidha, watuhumiwa 11 walikamatwa kwa makosa ya wizi wa pikipiki (bodaboda), wanne kwa wizi wa pikipiki za magurudumu matatu (bajaji).

"Baada ya ukamataji huo baadhi ya kesi zipo chini ya upelelezi, zingine zimefikisha mahakamani zikiendelea kusikilizwa na zipo zilizopata mafanikio kwa watuhumiwa kuhukumiwa vifungo mbalimbali," amesema.

Alisema baadhi ya mafanikio ya kesi zilizofikishwa mahakamani kwa kipindi hicho ni pamoja na Mustafa Hamis (35), kuhukumiwa kifungo cha maisha jela kwa kosa la kulawiti na kubaka, Musa Masanilo (35), amehukumiwa kwenda jela miaka 30 kwa kosa la kubaka na Baraka Yohana (23) amehukumiwa jela miaka 39 kwa kosa la kubaka.

Kamanda Kakwale alisema Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama barabarani limefanya doria na misako na kufanikiwa kuwakamata madereva wawili kwa makosa mwendesha magari kwa mwendokasi usioruhusiwa kisheria.

Aliwataja madereva waliokamatwa kuwa ni Athuman Kasenya (34), ambaye ni dereva wa basi lenye namba za usajiri T 454 DHP mali ya kampuni ya Matunduru na Julius Dionice (39), dereva wa basi la kampuni ya Satco lenye namba T 937 EFK.

"Kutokana na makosa hayo, madereva hao walifungiwa leseni zao za udereva kwa kipindi cha miezi mitatu kwa uendeshaji wa gari kwa njia ya hatari na isiyofaa jambo ambalo ni hatari kwa watumiaji wengine wa barabara," alisema.

---

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

## TANGAZO LA VIJANA KUJIUNGA NA VITUO VYA JENGA KESHO ILIYO BORA (BBT) VYA UFUGAJI MIFUGO KIBIASHARA

1. Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakaribisha maombi ya Vijana kujiunga na vituo vya BBT vya ufugaji mifugo kibiashara ambapo watakaa kwa kipindi kisichozidi Mwaka mmoja katika maeneo yafuatayo:-
   i. Uyui - Tabora
   ii. Makuyuni - Arusha
   iii. Mkata - Morogoro
   iv. Ruvu - Pwani
   v. Nangaramo - Mtwara

2. Waombaji watakuwa katika makundi matatu kama ifuatavyo:-
   i. Asilimia 40 ya vijana watakaodahiliwa watatoka katika Halmashauri za Mkoa husika ambapo Mradi utatekelezwa na maombi yatatumwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika (Anuani ya kila Katibu Tawala wa Mkoa husika imenakilishwa mwisho wa Tangazo hili),
   ii. Asilimia 30 ya vijana watatoka katika Jeshi la Kujenga Taifa na majina yao yatawasilishwa na Mkuu wa JKT kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika, na
   iii. Asilimia 30 ya wadahiliwa ni Vijana waliohitimu Mafunzo katika vyuo vya Mifugo kwa ngazi ya shahada, stashahada au cheti. Maombi katika kundi hili yaelekezwe kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika.

3. Sifa za waombaji
   i. Awe Raia wa Tanzania,
   ii. Awe na umri kati ya Miaka 18 – 30,
   iii. Mwombaji awe ni Kijana mwenye tabia njema na Barua yake ya maombi iidhinishwe na uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa anapoishi,
   iv. Awe tayari kushiriki mafunzo kwa vitendo katika shughuli za ufugaji mifugo kibiashara katika kipindi husika,
   v. Awe tayari kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa katika kituo atakachokuwa akifanyia shughuli za ufugaji kibiashara, na
   vi. Awe mwenye Afya njema itakayomwezesha kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mradi.

4. Fomu ya kujiunga na vituo hivi inapatikana kupitia tovuti za Wizara ya Mifugo na Uvuvi (**www.mifugouvuvi.go.tz**) na za Sekretarieti za Mikoa husika. Fomu ya Maombi kwa kundi namba 2(iii) iambatishwe nakala ya vyeti vya masomo vilivyothibitishwa. Aidha, waombaji wote wawasilishe nakala za vitambulisho vya NIDA vya mwombaji na nakala ya kitambulisho cha Mdhamini.

5. Fomu ya maombi na viambatisho vitumwe kupitia barua pepe za Mikoa husika.

6. Waombaji watakaochaguliwa katika hatua ya kwanza wataitwa kwa ajili ya usaili kwa vitendo katika vituo walivyochaguliwa. Waombaji wawe tayari kujigharamia nauli, chakula na malazi wakati wa usaili kwa vitendo vituoni.

7. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24/05/2024.

8. Maombi yawasilishwe kupitia barua pepe za Katibu Tawala wa Mikoa husika kama ifuatavyo:-

   Mkoa wa Tabora: **ras.tabora@tamisemi.go.tz**
   Mkoa wa Arusha: **ras@arusha.go.tz**
   Mkoa wa Morogoro: **ras.morogoro@tamisemi.go.tz**
   Mkoa wa Pwani: **ras@pwani.go.tz**
   Mkoa wa Mtwara: **ras@mtwara.go.tz**

   Kwa ufafanuzi zaidi, Wasiliana na:-
   i. Mkoa wa Tabora: Asanterabi Sangenoi **– 0754 – 450183 AU Mussa H. Mussa - 0682058815**
   ii. Mkoa wa Arusha: Dkt. Sabas P. Shange - **0756442966 AU Bw. Richard Nkini - 0754082195/0684057000**
   iii. Mkoa wa Morogoro: Dkt.Gasper Msimbe – **0652434368/0620279198 AU Bw. Waziri Mahimbo - 0714752134**
   iv. Mkoa wa Pwani: Elisante S.Qadwe – **0787302606 AU Dr. Ramadhani A. Mwaiganju - 0612600390**
   v. Mkoa wa Mtwara: Dr. Subira Simbeye **- 0785648115 AU Bw. Nanjiva Geofrey - 0655353051**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Haya yakitekelezwa kikamilifu sekta ya elimu italeta mageuzi

**WAZIRI** wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, jana aliwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 wenye vipaumbele vitano. Katika utekelezaji wa vipaumbele hivyo, vyenye lengo la kuimarisha ubora wa elimu nchini, Waziri Mkenda aliomba Bunge kupitisha Sh. trilioni 1.96.

Vipaumbele ambavyo vimeanikwa katika makadirio hayo ili kutekelezwa ipasavyo ni pamoja na ujenzi wa shule za sekondari za ufundi 100 ambazo 20 kati ya hizo zinatarajiwa kufunguliwa mwakani na kudahili wanafunzi. Lengo la ujenzi wa shule hizo ni kutoa elimu na mafunzo ya ufundi ili kuwawezesha vijana wengi kuwa na ujuzi ambao utawasaidia kuwa na uelewa mpana wa masomo ya ufundi ambao utachangia maendeleo ya sekta zingine.

Pia katika mwaka ujao wa fedha, serikali kupitia wizara hiyo, inatarajia kujenga shule mpya za amali (ufundi na ufundi stadi) katika maeneo ambayo hayana vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi au shule ya amali ya sekondari. Pia wanafunzi 263,718 wanatarajia kudahiliwa katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ambapo 190,518 ni wa elimu ya ufundi na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 73,200.

Sambamba na kipaumbele hicho, alisema serikali itaongeza fursa za utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wenye sifa na uhitaji kutoka 223,201 hadi 252,245 wakiwamo 84,500 wa mwaka wa kwanza ambao watanufaika na mikopo hiyo.

Vipaumbele vingine, kwa mujibu wa Waziri Mkenda ni kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria na kuandaa miongozo ya utoaji elimu na mafunzo nchini na pia kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, kuimarisha ubora wa elimu ya msingi, sekondari na ualimu.

Kadhalika, alisema katika mwaka ujao wa fedha, serikali itafanya mapitio ya mitaala 171, kuandaa mitaala mipya 18, kuanzisha programu za vipaumbele 145 na matumizi ya mbinu bunifu za ufundishaji katika elimu ya juu.

Jambo lingine alilolibainisha ni kuipa nguvu Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ili kusimamia kikamilifu utoaji na urejeshwaji wa mikopo pamoja na kufungua mashauri dhidi ya wale wanaokiuka utaratibu wa urejeshaji wa mikopo hiyo.


Ni dhahiri kwamba vipaumbele hivyo vinajibu maswali kuhusu ubora wa elimu nchini ambao umekuwa ukikosolewa mara kwa mara na wadau. Moja ya mambo ambayo yamekuwa yakilalamikiwa ni mitaala ya elimu ambayo imekuwa haiendani na hali halisi ya sasa katika soko la ajira.

Wadau hao wamekuwa wakidai kuwa mitaala iliyopo imejikita katika nadharia zaidi kuliko vitendo hali ambayo inasababisha vijana wengi wanaohitimu kutoajirika katika sekta mbalimbali au kujiajiri. Katika hilo, serikali imejibu kwa kuboresha mitaala na kuanzisha elimu ya ufundi na mafunzo ya amali ili kuwezesha vijana wengi kuwa na ujuzi wa fani anuai utakaowasaidia kujiajiri na kupunguza tatizo la ajira nchini.

Kilio kingine ambacho kimekuwapo kwa muda mrefu ni wanafunzi kukosa mikopo ya juu licha ya kuwa na sifa. Serikali inastahili pongezi kwa kuwa suala hilo limeainishwa kama moja ya vipaumbele na wanufaika wa mikopo hiyo wataongezeka katika mwaka ujao wa masomo ya elimu ya juu.

Hata hivyo, kupanga ni jambo moja na utekelezaji ni jambo lingine. Kwa mantiki hiyo, jambo la muhimu ni wizara kutekeleza mipango kama ilivyoainishwa katika makadirio hayo na pia serikali kutoa kwa wakati fedha kwa mujibu wa bajeti kwenye sekta hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Bunge lisisahau kujadili maafa

Na Gaudensia Mngumi

**MABADILIKO** ya tabianchi ni bayana au hakika. Si hadithi za kusimuliwa tena. Watu wameona kwenye televisheni, mitandao ya kijamii lakini wapo Watanzania wenzetu wakazi wa Rufiji.

Wanaoishi maeneo ya Mloka, Utete na Ikwiriri wameshuhudia mafuriko makubwa yaliyoumiza familia nyingi kuanzia kupoteza maisha na mali.

Ni ukweli kuwa Tanzania sasa inakuwa eneo la kukabiliwa na mafuriko, kimbunga, tufani, dhoruba na hata jua na joto kali au baridi kali na sasa ni wakati wa kujiandaa na kuweka uhimilivu.

Bunge la Bajeti linavyoendelea Dodoma, huenda itapendeza kama litaongeza muda na kuweka sawa masuala ya majanga kama ambavyo taifa limeshuhudia.

Ni vyema pia kutoa mafunzo na kuongeza zaidi bajeti na wataalamu wa masuala ya maafa kwa sababu kiasi miaka inavyosonga hili linakuwa janga la kitaifa.

Ikumbukwe kuwa kiasi miaka inavyokwenda ndivyo nchi itakavyokabiliwa na mafuriko mabaya na makubwa zaidi, kama maporomoko ya ardhi.

Haya yameshuhudiwa yakiathiri maisha ya watu huko Hanang' mkoani Manyara na Kawetere mkoani Mbeya.

Ni vyema Watanzania wakafahamu ukweli kuwa hakuna sehemu yoyote ya nchi yao ambayo inaweza kusema iko salama na ina kinga dhidi ya mafuriko na maafa ya majanga ya kiasili.

Kuna kimbunga mathalani cha Hidaya ambacho kilileta upepo mkali wiki iliyopita ambao ungeweza kuwa mkali na kasi zaidi ukaangusha miti, nguzo na nyaya za umeme, kuezua mabati na kubomoa majengo pamoja na kuua watu.

Upepo huo kama ungeambatana na mvua ni wazi kuwa matokeo yake yangekuwa ni athari zaidi, hivyo ni wazi kuwa hali ya hewa inabadilika kila wakati na huenda inatarajiwa kuwa mbaya zaidi katika siku zijazo na kunatarajiwa kuwa athari mbaya zaidi pia.

Ni wazi kuwa kimbunga Hidaya kimeipiga Mtwara na Mafia, kimesababisha mvua kubwa, upepo mkali na mawimbi makali na hatari baharini.

**Wanaoishi maeneo ya Mloka, Utete na Ikwiriri wameshuhudia mafuriko makubwa yaliyoumiza familia nyingi kuanzia kupoteza maisha na mali.**

Mambo yote haya yameleta athari kwanza vifo na majeruhi, kuharibu makazi, mazao, kukwamisha na kutatiza shughuli za kiuchumi kuanzia uvuvi baharini , usafiri mfano kubomoka na kuharibiwa daraja la Mto Matandu wilayani Kilwa.

Ndiyo maana ni wakati wa Bunge kuamua namna bora ya kujihami na vimbunga kama Hidaya na Jobo ambavyo huathiri ufukwe wa Bahari ya Hindi na makazi katika pwani ya Tanzania kuanzia Tanga hadi Mtwara.

Serikali lazima ichukue hatua madhubuti sasa na haraka ili kupunguza athari mbaya za athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo hayatabiriki.

Suala la elimu ni muhimu kuangaliwa ikibidi shule ziangaliwe zilizoko mtoni ikiwezekana zifungwe kwa muda au zihamishwe kuondoa uwezekano wa watoto kupoteza maisha wakati mvua kubwa zinaponyesha.

Umeme ni suala la kuangaliwa zaidi tena kwa jicho pevu kwa kuwa kimbunga ambacho ni upepo mkali kinaweza kuangusha miti kung'oa nguzo za umeme, kuharibu nyaya na vifaa vyote vya kusafirishia umeme mijini na vijijini. Janga hilo linaweza kuitumbukiza nchi katika giza kuu.

Hilo nalo ni suala la kuangaliwa kwa sababu kimbunga hakimwachi yeyote salama, hata taasisi nyeti kama sekta ya umeme haziko salama.

Kuchukua tahadhari ni pamoja na kuhakikisha kuwa kuna mashine au mitambo ya za kufua umeme kwa dharura, magari, helkopta, dawa, huduma za dharura iwe ni kuondoa vifusi barabarani karibu kila mahali ili kupunguza athari za mafuriko mijini na vijijini pia.

Ikumbukwe kuwa uharibifu wa maafa kama hayo huwaacha watu bila makaazi na huduma muhimu kama maji, chakula na mavazi hilo nalo liangaliwe kwenye mijadala ya bunge ya kukabiliana na maafa na taifa kujiwekea mpango wa dharura wa kujihami na kuhimili.

HABARI KITAIFA

# Wanawake wahamasishwa kuchukua fomu kuwania uongozi

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MTAKWIMU Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, amewataka wanawake nchini kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu na Uchaguzi Mkuu 2025 ili kufikia idadi ya 50 kwa 50.

Alisema hayo juzi kwenye semina ya viongozi kuhusu mafunzo ya usambazaji na matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi 2022, iliyofanyika wilayani Iramba, mkoani Singida.

Dk. Chuwa alisema kutokana na takwimu za Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika 2022 zinaonesha wanawake ni wengi nchini hivyo ni vyema wakatumia wingi huo kuchukua fomu kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kwa kuanzia na uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa katika Wilaya ya Iramba wanawake wanaongoza kwa sababu wapo 165, 000 huku wanaume wakiwa 163,000.

"Wanawake wenzangu tuna kazi, tumesoma, tuna sera ya 50 kwa 50, hivyo tukachukue fomu kuwania uongozi kwa sababu takwimu zimekwishatuonesha tupo wengi," alisema Dk. Chuwa.

Aidha, kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya 2022 inaonyesha kuwa kiwango cha watu kuanzia umri wa miaka mitano na kuendelea wanaojua kusoma na kuandika kimeongezeka hadi asilimia 83.

Alisema kuwa wamepiga hatua kufikia kiwango hicho ikilinganishwa na asilimia takribani 44 kipindi cha Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Kadhalika, Mkoa wa Singida una asilimia 70 huku kwa Wilaya ya Iramba wakiwa asilima 68 ya watu wanaojua kusoma na kuandika kwa lugha yoyote.

Dk. Chuwa alisema hatua hiyo ni kubwa na kuwataka viongozi kuungana na serikali yao kwa kwenda kufanyia kazi takwimu hizo kwa lengo la kuleta maendeleo nchini.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alisema wilaya hiyo imepiga hatua kubwa kimaendeleo na wakati anateuliwa kuiongoza Iramba, alikuta vijiji 54 ndio vyenye umeme na sasa vijiji vyote 70 vya wilaya hiyo vina umeme.

Alisema kuwa vitongoji 189 vina nishati hiyo na kuwa wananchi hao wanapata ruzuku toka serikalini wanapolima.

"Furaha ya mara mbili wanayoionesha wananchi wangu imeletwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye anabebwa na takwimu zinazoeleza mambo mbalimbali aliyoyafanya nchini," alisema.

Mjumbe wa Baraza Kuu Taifa la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), anayewakilisha wanawake wa Mkoa wa Singida, Grace Mkoma, amemshukuru Dk. Chuwa kwa kutoa elimu itokanayo na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Mkoma aliwataka viongozi walionufaika ma mafunzo hayo kwenda kuyafanyia kazi yote waliofundishwa ikiwamo kuifikishia jamii.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi wa CCM Kata ya Ilala, Sabry Shariff akichangia damu kwa ajili ya wahitaji katika kilele cha Wiki ya Wazazi, katika viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: PILLY KIGOME**

# Bil. 11/- zalipwa kifuta machozi waathirika wa wanyamapori

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema kwa kipindi cha miaka saba Sh. bilioni 11.08 zimelipwa kama kifuta jasho na machozi kwa wananchi walioathirika na wanyama wakali na waharibifu.

Hata hivyo, Wizara ya Maliasili na Utalii ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na Wizara ya Fedha ili kupata ridhaa ya matumizi ya viwango vipya vya fidia kwa kuwa viwango vilivyopo sasa vimepitwa na wakati.

Naibu Waziri, Danstan Kitandula, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Naghenjwa Kaboyoka.

Katika swali lake, Mbunge huyo aliyetaka kujua, katika kipindi hicho cha miaka saba (2017 - 2022) ni kiasi gani cha fedha kimelipwa kama kifuta jasho kwa uharibifu wa mazao na watu kuuliwa na tembo.

Kitandula alisema kiasi hicho cha fedha ni kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi Machi, 2024. Aidha, alisema tayari wizara imezifanyia marekebisho kanuni za kifuta jasho na machozi na kwasasa ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na Wizara ya Fedha ili kupata ridhaa ya matumizi ya viwango vipya vya fidia kwa kuwa viwango vilivyopo sasa vimepitwa na wakati.

Alifafanua kuwa serikali imekuwa ikijitahidi kulipa fedha hizo kwa wakati inapopata taarifa kutoka kwenye halmashauri za wilaya na mchakato wa tathmini kufanyika ili kujua gharama halisi ya fedha inayotakiwa kulipwa.

Alisisitiza kuwa serikali imeendelea kufanya jitihada mbalimbali za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa kujenga vituo vya askari kwenye makazi ya wananchi ili kuwasogeza karibu na maeneo yenye changamoto.

"Moja ya jitihada zilizofanywa na serikali ni kujenga vizimba vya kuzuia mamba wasidhuru wananchi wanapotumia maji ya mito au maziwa, pia kuandaa mfumo wa kielektroniki ili kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu," alisema.

Pia alisema imeweka namba maalum za simu kwenye vituo vya kanda za kiutendaji za taasisi za uhifadhi kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kutoa taarifa za matukio ya wanyamapori bila malipo.



# TAKUKURU yatoa kauli uchunguzi madai fedha chafu CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU), imesema bado inaendelea kuchunguza madai ya fedha chafu ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), yaliyotolewa na Makamu Mwenyekiti Bara, Tundu Lissu, Mei 3, mwaka huu.

Nipashe ilimtafuta Mkuu wa TAKUKURU nchini, Salum Hamdani kutaka kujua uchunguzi wa jambo hilo umefikia wapi baada ya TAKUKURU kutangaza kufanya uchunguzi baada ya kiongozi huyo kutoa shutuma dhidi ya chama chake akiwa kwenye mkutano wa hadhara mjini Iringa.

"Uchunguzi ni 'process' na inachukua muda, kwa hiyo taarifa tumeipokea na tunaifanyia kazi, siwezi kusema itachukua muda gani lakini tunaifanyia kazi," alisema Hamduni.

Aidha, juzi katika ukurasa wa X, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema aliyenukuu kauli iliyoandikwa na mmoja wa wanachama wa chama hicho kikuu cha upinzani Tanzania, Bob Wangwe.

Katika akaunti yake ya X, Lema aliandika kwamba, "Nimeona andiko la BOB Wangwe na maandiko mengine ya watu wengi pamoja na ushauri wake."

"Jibu langu kwenu ni hili, tukiwa Arusha mahali fulani kwenye mazungumzo yetu ambapo nilikuwapo pamoja na kamanda Heche, Msigwa na Mwenyekiti Mbowe, Lissu aliongea maneno haya nanukuu "Kaka, Mwenyekiti, ulibeba chupa ya damu nisife wakati nimeshambuliwa kutoka Dodoma ukiwa umesimama kwenye ndege mpaka Nairobi."

"Na ulikaa Nairobi na wenzako hawa muda wote wa matibabu yangu, siwezi kuchukua fomu utakayogusa kwenye chama hiki, tusiruhusu wapambe watuharibie chama."

Lema aliandika kwamba maneno hayo aliwahi kuyasema Lissu wakiwa na John Heche, Peter Msigwa na Ezekiel Wenje pamoja na Mbowe.

Aidha, alisema hakuna vita kwenye nafasi ya urais ndani ya CHADEMA isipokuwa kuna wapambe hasa katika mwelekeo wa siasa wa mwaka 2024 na 2025.

Katika ukurasa wake wa X, Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Kichama Kinondoni aliandika: "Kelele za WanaCCM dhidi ya CHADEMA ni jambo la kawaida kwenye siasa za ushindani. CCM haiwezi kushambulia chama kingine cha siasa zaidi ya CHADEMA kwa kuwa inajua CHADEMA ndiyo tishio kwao. Hivyo hivyo kwa CHADEMA haiwezi kuhangaika na vyama vingine isipokuwa CCM. Tuishi humu."

Hoja ya Lema na Kileo imekuja kukiwa na mjadala mitandaoni kuhusu kauli zilizotolewa na Lissu hivi karibuni na mojawapo akidai kwamba ndani ya chama hicho kuna fedha chafu.

Akiwa katika moja ya mikutano yake hivi karibuni mkoani Iringa, Lissu alitamka kauli hiyo akidai kwamba fedha hizo chafu hazijulikani zimetoka wapi.

"Kuna mtafaruku mkubwa sana wa uchaguzi ndani ya chama chetu. Kuna pesa nyingi ajabu kwenye uchaguzi huu, hela ambayo tukisema tufanye mikutano, tutafute vyombo vya matangazo huwa haipo.

"Leo kwenye uchaguzi kuna hela ya ajabu, nyinyi mnafikiri hii hela ni ya wapi, mnafikiri hii hela itatuacha salama? Ukitaka kujua hatuko salama fuatilia mitandaoni, hizo pesa si za CHADEMA kwa sababu sisi huwa hatuna hela zozote," alisema Lissu.

Kwa sasa chama hicho kinaendelea na chaguzi za ndani ya chama katika ngazi ya kanda ambazo baadhi zimeonyesha kuwa na ushindani mkali na wanaojadili mtandaoni wanasema huenda wagombea kwenye kanda husika wana majibu ya kauli hiyo ya Lissu.

Baadhi ya Kanda za CHADEMA zinazotarajia kuwa na uchaguzi ni Kanda ya Nyasa, Victoria, Kati, Kusini, Kaskazini, Pwani na Magharibi.




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (wa pili kushoto), akipata maelezo ya mradi mpya wa nyumba za bei nafuu wa Sky Royal kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hainan International Ltd, Zhou Tao (wa pili kulia), baada ya kuuzindua mradi huo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkurugenzi wa Kanda wa Kampuni ya RE/MAX, Joseph Prevost. **PICHA: WANMM**

## Bilioni 19/- zahitajika kukarabati miundombinu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SHILINGI bilioni 19 zinahitajika kurejesha hali stahimilivu ya miundombonu ya barabara za mijini na vijijini iliyoharibiwa na mvua za El-nino kwenye wilaya mbalimbali mkoani hapa.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Ndyamukama, alisema hayo jana wakati akiongea na waandishi wa habari kuwa katika uharibifu wa mwanzo serikali ilitoa Sh. bilioni 2.8 ambazo utekelezaji wake ulikwama kutokana na mvua kuwa kubwa.

Mhandisi Ndyamukama alisema utekelezaji wa ukarabati wa miundombinu ya barabara hizo utaanza baada ya hali kukaa sawa ndani ya mwezi Mei kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA).

Alisema mvua inayoendelea kunyesha imeharibu sehemu kubwa ya miundombinu kwenye mkoa hasa katika wilaya za Ulanga, Kilombero, Malinyi na Mlimba na kuvuruga utaratibu wa kawaida wa matengenezo ya barabara waliojiwekea.

Aidha, Mhandisi Ndyamukama alisema katika mwaka wa fedha 2023/24 mkoa ulipokea bajeti ya barabara ya Sh. bilioni 26 kwa ajili ya kutekeleza maboresho ya barabara fedha zilizotoka Serikalini kupitia fedha za mfuko wa barabara, mfuko wa jimbo na mfuko wa tozo.

Alisema wakati wakiwa karibu asilimia 50 ya utekelezaji wa mpango wa kawaida wa maboresho ya barabara ndipo mkoa ukakumbwa na changamoto ya El-nino na kusababisha utekelezaji wa bajeti husika kusimama.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga mkoani hapa, Edson Wiliamsoli, aliiomba TARURA na TANROADS kuongeza juhudi za kukarabati miundombinu hiyo ili kurejesha mawasiliano katika maeneo mbalimbali ikiwamo daraja la eneo la Ketaketa ambalo awali lilijengwa na TARURA na kugharimu Sh. milioni 700, lakini kwa sasa limekatika.

Aliyataja madaraja mengine yaliyokatika kuwa ni ya kwenye maeneo ya Ngongo, Mwaya na Libenanga na nguvu za wananchi akiwamo mbunge wa jimbo hilo Hasham Alaudin kuweka mawe kwenye baadhi ya maeneo zilisaidia baadhi ya maeneo kupitika kiasi.

# Mbunge ashauri kuondolewa dhamana wanaobaka, kulawiti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko, amesema moja ya sababu inayochangia kukithiri kwa matukio ya watoto kubakwa na kulawitiwa ni kutokana na watuhumiwa kupewa dhamana na wanaporejea mtaani huharibu ushahidi.

Matiko alishauri watuhumiwa hao wasipewe dhamana kama ilivyo kwa makosa mengine ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Akitoa ufafanuzi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi alisema, kwa mujibu wa sheria makosa yaliyotungiwa sheria bungeni ndio yanakuwa makosa ya jinai.

"Baada ya maswali kuwa mengi kwenye bunge hili, mwaka jana bunge lilielekeza serikali ifanye utafiti wa kina kupitia Tume ya Marekebisho ya Sheria na kazi hii inaendelea," alisema.

Alisema yote ambayo yanaendelea, yanahusisha jamii na makundi mbalimbali na hakuna tofauti yoyote kwa sababu uhalifu unapofanyika mtoa taarifa anatakiwa kutoa taarifa yake kwa mujibu wa kifungu cha saba cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai.

Alibainisha kuwa baada ya taarifa ya jinai kutolewa upepelezi huwa unaanza na suala la dhamana linashughulikiwa kwa mujibu wa kifungu cha 148 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya mashauri ya jinai.

Alifafanua kuwa kuna mazingira ya kupinga dhamana Mwendesha Mashitaka ambaye anaiwakilisha Jamhuri anawasilisha pingamizi kwa mujibu wa sheria na linasikilizwa.

"Wapo wengi ambao hawapewi dhamana kwa sababu ya vitendo walivyovifanya vipo kinyume na kustahilisha wao kupewa dhamana, hivyo dhamana ni haki ya kikatiba na kwa mujibu wa sheria isipokuwa kwa makosa ambayo kifungu cha 148(5) imezuia makosa hayo yasidhaminike," alisema.

Alisema makosa yoyote yanayodhaminika dhamana hupingwa kwa kuendana na mazingira hayo ambayo hulazimika mahakama yenye dhamana ipewe hoja na ifanye maamuzi.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Singida Kaskazini (CCM), Ramadhan Ighondo alitaka kujua serikali ina mkakati gani wa kukomesha ukatili dhidi ya watoto.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ally Khamis, alisema wizara kwa kushirikiana na wizara za kisekta inaratibu utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na tatizo la mmomonyoko wa maadili na ukatili dhidi ya watoto.

Aliitaja mikakati hiyo ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto pamoja na kuanzisha na kuimarisha madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za msingi, sekondari na vyuo.

Mkakati mwingine ni kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) pamoja na Mpango wa Taifa wa Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (NAIHA).

"Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma na kuongeza afua za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto pamoja na kuimarisha taasisi ya familia kwa lengo la kupunguza au kumaliza kabisa changamoto ya mmomonyoko wa maadili nchini.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MUHTASARI WA HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF F. MKENDA (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025



**Prof. Adolf Faustine Mkenda**
Waziri



**QS. Omari Juma Kipanga**
Naibu Waziri



**Dkt. Franklin Jason Rwezimula**
Naibu Katibu Mkuu



**Prof. Carolyne Ignatius Nombo**
Katibu Mkuu



**Prof. James Epiphan Mdoe**
Naibu Katibu Mkuu





# MUHTASARI WA HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF F. MKENDA (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025

**A. UTANGULIZI**

**1.** Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya FUNGU 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na FUNGU 18 - Tume ya Taifa ya UNESCO, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa mwaka wa fedha 2023/24. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

**2.** Mheshimiwa Spika**,** awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo kujadili utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24 na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Taifa ya UNESCO kwa mwaka wa fedha 2024/25.

**3.** Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, na Watanzania wote kwa kuondokewa na kiongozi wetu mpendwa **Hayati Ali Hassan Mwinyi** aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika tutaendelea kumuenzi kwa mchango wake mkubwa katika mageuzi ya kisiasa, kiuchumi na kielimu hususan kwa kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu nchini.

**4.** Mheshimiwa Spika**,** vilevile, ninaomba kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote kwa kuondokewa na **Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa** aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakumbukwa kwa uchapakazi na umahiri wake katika usimamizi wa kazi za Serikali ikiwemo uanzishaji wa Shule za Sekondari za Kata zilizoongeza fursa ya elimu ya sekondari nchini.

**5.** Mheshimiwa Spika, niungane na wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil (Mb) aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani Zanzibar ambaye pia alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo.

**6.** Mheshimiwa Spika**,** ninaomba kuhitimisha salamu zangu za pole kwa kutoa pole kwa Watanzania wote waliopoteza ndugu na jamaa na kupoteza au kuharibikiwa na mali kutokana athari za mvua kubwa zinazoendelea nchini. Mwenyezi Mungu awape marehemu pumziko la milele, Amina! Aidha, tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji majeruhi wote ili waweze kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa letu.

**7.** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu ya uongozi ulio mahiri na wenye weledi mkubwa. Katika kipindi cha miaka mitatu, Mheshimiwa Rais ametuongoza katika kupata mafanikio makubwa nchini ikiwemo mageuzi katika mfumo wa elimu na mafunzo yanayolenga kuandaa nguvu kazi yenye maarifa, stadi na mtazamo chanya katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa letu. Aidha, natoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo yake yaliyotusaidia katika kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na kufanya marekebisho kwenye mitaala ili kutoa elimu ujuzi kulingana na mazingira ya nchi na soko la ajira.

**8.** Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini mimi pamoja na Mheshimiwa Omary Juma Kipanga (Mb) Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuongoza Wizara hii.

**9.** Mheshimiwa Spika, vilevile, ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb) Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao mahiri katika kuliongoza Taifa letu.

**10.** Mheshimiwa Spika, ninapenda kukupongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani; Mwanamke wa tatu kushika nafasi hiyo duniani na wa kwanza kutoka Afrika. Vilevile, ninakupongeza Mheshimiwa Spika pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa. Natumia nafasi hii pia kuwapongeza wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama Mbunge wa Madaba na Mheshimiwa Deo Mwanyika Mbunge wa Njombe Mjini kwa umakini wao katika kuliongoza bunge lako Tukufu.

**11.** Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Zainabu Athuman Katimba (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**12.** Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Makamu Mwenyekiti Musa Ramadhani Simma na wajumbe wote wa Kamati. Aidha, naomba niwashukuru kwa kupokea, kuchambua na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2023/24 na kuishauri vema Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2024/25. Natambua na kuthamini sana mchango wa Kamati katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inachangia katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano 2021/22 – 2025/26 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 kwa kuandaa rasilimaliwatu yenye ujuzi, maarifa na stadi zitakazowezesha kujenga uchumi shindani wa viwanda na kuendelea kustawisha maisha ya kila Mtanzania, kutokomeza umasikini na kuhakikisha kuwa Taifa linafikia uchumi wa kati.

**13.** Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wananchi wa Jimbo la Rombo kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu hasa mke wangu mpendwa Profesa Beatrice kwa kuendelea kuwa karibu yangu na kunitia moyo na kuniwezesha kufanya kazi kwa juhudi na ari kubwa.

**14.** Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya utelekezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.

**B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI**

**15.** Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,675,753,327,000.00** kwa ajili ya FUNGU 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo **Shilingi 537,880,762,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,137,872,565,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - FUNGU 18 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 2,733,888,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha **Shilingi 1,124,980,000.00** za Mishahara na **Shilingi 1,608,908,000.00** za Matumizi Mengineyo.

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

**16.** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara kupitia FUNGU 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 679,362,572,548.64** ambapo kiasi cha **Shilingi 11,660,695,000.00** kilipangwa kukusanywa na idara na vitengo na **Shilingi 667,701,877,548.64** zilipangwa kukusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli hayo ni kutokana na ada, malipo ya ushauri elekezi, huduma za Uthibiti Ubora wa Shule na utoaji wa huduma mbalimbali.

**17.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 15, 2024 Wizara imekusanya **Shilingi 397,598,746,452.42** sawa na **asilimia 59** ya makadirio ambapo **Shilingi 11,072,869,322.29** zimekusanywa na idara na vitengo na **Shilingi 386,525,877,130.13** zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Matumizi ya Kawaida**

**18.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 537,880,762,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya mishahara ni **Shilingi 500,957,569,000.00** (idara na vitengo **Shilingi 83,200,218,000.00** na Taasisi ni **Shilingi 417,757,351,000.00)** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 36,923,193,000.00** (idara na vitengo ni **Shilingi 26,416,806,658.00** na Taasisi **Shilingi 10,506,386,342.00**).

**19.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 15, 2024, Wizara imepokea Jumla ya **Shilingi 405,900,247,712.40** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46 sawa na **asilimia 75** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO – Fungu 18 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,906,916,317.62** sawa na **asilimia 70** ya fedha ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**Miradi ya Maendeleo**

**20.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,137,872,565,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi 979,083,678,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 158,788,887,000.00.**

**21.** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili 15, 2024, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 988,594,227,608.28** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 87** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 900,697,116,186.31** ni fedha za ndani na **Shilingi 87,897,111,421.97** ni fedha za nje.

**C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA**

**22.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitekeleza vipaumbele vitano ambavyo ni:

(i) kukamilisha Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu na kuanza utekelezaji wake kwa lengo la kuimarisha ujuzi kwa wahitimu;

(ii) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali (ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) kwa sekondari na vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(iii) kuwezesha Ongezeko la fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya msingi, sekondari na ualimu;

(iv) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na

(v) kuimarisha uwezo wa nchi katika tafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

**a. Kuhuisha Sera na Sheria, na Utoaji wa Miongozo ya Elimu na Mafunzo Nchini.**

**1.** Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na kuandaa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023. Vilevile, tumefanya mabadiliko makubwa na kuboresha mitaala ya elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu ya sekondari, pamoja na mafunzo ya ualimu. Utekelezaji wa mitaala mipya imeanza kwa awamu kuanzia Januari 2024. Aidha, katika kuhakikisha mitaala inatekelezwa kwa ufanisi, Serikali imetoa Waraka wa Elimu Na. 5 wa mwaka 2023 wenye kutoa mwongozo wa utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa ili kurahisisha utekelezaji wake. Uboreshaji wa sera na mitaala utaimarisha utoaji wa elimu na kuwezesha wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kupata elimu bora zaidi kitaaluma na pia yenye ujuzi na maarifa yenye kuendana na mipango ya nchi na mahitaji ya kitaaluma na ajira.

**2.** Mheshimiwa Spika, ili mitaala iliyoboreshwa iweze kutekelezwa ipasavyo Serikali imewajengea uwezo walimu na wasimamizi kuhusu utekelezaji wa mitaala kama ifuatavyo:

(i) imetoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa kwa wawezeshaji 11,521 wa kitaifa ambao ni; walimu weledi wa darasa la awali, maafisa elimu kata, wathibiti ubora wa shule; na walimu weledi kutoka taasisi mama zinazomiliki shule zisizo za Serikali, wakuza mitaala na wakufunzi;

(ii) imewajengea uwezo viongozi wa elimu 569 wakiwemo maafisa elimu wa mikoa, maafisa elimu msingi, maafisa elimu taaluma, maafisa elimu wa elimu maalum na wathibiti ubora wa shule kuhusu usimamizi na utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa;

(iii) imetoa mafunzo kwa walimu 182,697 sawa na asilimia 81 ya walimu wa awali na msingi kuhusu mitaala iliyoboreshwa wakiwemo walimu 155,476 wa shule za Serikali, 26,301 wa shule zisizo za Serikali, na walimu 920 wanaofundisha

wanafunzi wenye mahitaji maalum waliofundishwa kuhusu mitaala iliyoboreshwa na utoaji wa elimu jumuishi;

(iv) imetoa mafunzo kuhusu Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la English na Sayansi kwa walimu wa shule ya msingi 70,717 (shule za Serikali 69,872 na shule zisizo za Serikali 845);

(v) imetoa mafunzo ya walimu 346 (walimu wa shule za Serikali 147 na zisizo za Serikali 199) wa Kidato cha Kwanza Mkondo wa Amali katika shule 96 (shule za Serikali 28 na zisizo za Serikali 68) ambazo zimeteuliwa kuanza kutekeleza Mtaala wa Amali Mwaka 2024;

(vi) imetoa mafunzo kwa walimu 428 wanaofundisha masomo ya Historia ya Tanzania na Maadili, English, Elimu ya Biashara na Hisabati katika shule 96 za sekondari zilizoteuliwa kutekeleza mtaala kwa kidato cha kwanza Mkondo wa Amali; na

(vii) imechapa na kusambaza nakala 9,818,251 za mihtasari, vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu kwa mchanganuo ufuatao: nakala 509,582 za mihtasari na mitaala iliyoboreshwa wa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari, nakala 8,074,326 za vitabu vya kiada vya kimacho kwa darasa la awali, darasa la I na la III, nakala 43,785 za vitabu vya maandishi yaliyokuzwa kwa darasa la awali, darasa la I na la III, nakala 6,990 za vitabu vya breli, nakala 1,183,568 za viongozi vya mwalimu na nakala za vitabu 6,900 vya masomo ya amali kwa kidato cha kwanza katika shule 96 (Serikali 28 na zisizo za Serikali 68).

**23.** Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa miongozo mbalimbali ili kuwezesha utekelezaji wa Sera na Mitaala. Miongozo hiyo ni:

(i) Mwongozo wa Shule ya Nyumbani; Mwongozo wa Ziara ya Nyumbani; Mwongozo wa Ubainishaji na Upimaji wa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum, Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Elimu pamoja na Mwongozo wa Utoaji wa Huduma za Kielimu Maalum kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum ili kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi nchini. Aidha, wanafunzi 429 wenye kiwango cha juu cha mahitaji maalum na changamoto ya afya wanafundishwa masomo mbalimbali na kupata huduma ya utengamao na uchechemuzi wakiwa nyumbani; na

(ii) Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika Shule za Awali, Msingi na Sekondari Tanzania Bara.

**b. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali (Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi) kwa Shule za Sekondari na Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**24.** Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu kwa ajili ya kuboresha mafunzo ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imebainisha shule 96 za sekondari (shule za Serikali ni 28 na zisizo za Serikali ni 68) ambazo zimeanza kutekeleza mitaala ya amali mwaka 2024;

(ii) imekamilisha ujenzi wa vyuo 29 vya mafunzo ya ufundi na ufundi stadi kati ya hivyo 25 ni vya wilaya na vinne ni vya kiwango cha mkoa. Vyuo 25 vya VETA vya Wilaya vimeanza kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Aidha, Serikali imetoa vifaa vya kufundishia, mitambo na kompyuta 20 kwa kila chuo kwa lengo la kuimarisha mafunzo kwa vitendo;

(iii) imeanza ujenzi wa Vyuo 64 vya VETA vya Wilaya kikiwemo chuo cha VETA Chamwino ambapo ujenzi wa chuo hicho umefikia asilimia 83. Kadhalika Serikali imejenga chuo cha VETA cha kiwango cha mkoa wa Songwe. Ujenzi huo unajumuisha majengo 18 kwa kila chuo cha Wilaya na majengo 25 kwa chuo cha Mkoa. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa karakana nne kwa ajili ya fani ya umeme, ufundi bomba, ujenzi na ufundi magari katika Chuo cha VETA cha Kihonda ambapo ujenzi umefikia asilimia 25. Aidha, imekamilisha ujenzi wa awamu wa kwanza ya Chuo cha Ufundi Dodoma chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 3000.

(iv) imekamilisha ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 436 katika Chuo cha Ufundi Arusha; ujenzi wa madarasa 10 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,800 katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Kampasi ya Pemba ambapo ujenzi umefikia asilimia 85 pamoja na hosteli mbili zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 768 kila moja katika Kampasi ya Karume Zanzibar ambapo ujenzi umefikia asilimia 49.

**25.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za mafunzo ya amali kupitia vyuo vya Amali kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeongeza udahili katika vyuo vya elimu ya ufundi (technical education and training colleges) kutoka wanafunzi **171,581** (wanawake 93,684) mwaka 2022/23 hadi wanafunzi **235,804** (wanawake 114,079) mwaka 2023/24. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa idadi ya vyuo vya elimu ya ufundi kutoka vyuo **465** (visivyo vya Serikali 285) mwaka 2022/23 hadi vyuo **474** (visivyo vya Serikali 294) mwaka 2023/24; na

(ii) imeongeza uandikishaji wa wanachuo katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi (vocational education and training colleges) kutoka wanafunzi **380,748** (wanawake 155,127) mwaka 2022/23 hadi wanafunzi **454,937** (wanawake 171,865) mwaka 2023/24. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi kutoka **687** (visivyo vya Serikali 563) mwaka 2022/23 hadi kufikia vyuo **830** (visivyo vya Serikali 705) mwaka 2023/24.

**26.** Mheshimiwa Spika, katika eneo la ithibati na uthibiti wa mafunzo ya amali (ufundi na mafunzo ya ufundi stadi), Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imesajili vyuo 29 katika bodi za masomo zifuatazo: Afya na Sayansi Shirikishi vyuo vinne; Biashara, Utalii na Mipango vyuo nane; Bodi ya Sayansi na Teknolojia Shirikishi vyuo vinne na vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi 13. Aidha, imetoa ithibati kwa vyuo 40 katika bodi za masomo zifuatazo: Afya na Sayansi Shirikishi vyuo 16; Biashara, Utalii na Mipango vyuo 17 na Sayansi na Teknolojia Shirikishi vyuo saba pamoja na programu 12 za ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(ii) imetoa Namba za Uhakiki wa Tuzo (AVN) 57,158 kwa lengo la kuimarisha uhakiki wa taarifa mbalimbali za wahitimu wa stashahada wanaoendelea na Elimu ya Juu pamoja na kuviwezesha vyuo kuhakiki udahili unaofanywa na Tume ya Vyuo Vikuu;

(iii) imehakiki mitaala 117 kati ya 230 iliyoandaliwa na Vyuo vya Ufundi kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira kwa wahitimu; na

(iv) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu katika shule za Amali 96 na Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi 108 kati ya lengo la vyuo 400. Aidha, shule na vyuo vilipewa ushauri wa namna ya kuboresha utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Vyuo ambavyo havikukidhi vigezo vilichukuliwa hatua stahiki ikiwemo kuvisimamisha na/au kuvifutia usajili ili kuvipa nafasi ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika.

**27.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na Taasisi na Mashirika mbalimbali katika utoaji wa mafunzo kwa vitendo katika Vyuo vya Ufundi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea kushirikiana na taasisi na mashirika 22 kutoka sekta rasmi na kutoa fursa ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 1,128 (wanawake 307) na walimu 23 (wanawake 3) kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wa mafunzo ya amali wanapata ujuzi na umahiri utakaowawezesha kujiajiri na kuajiriwa; na

(ii) imeanza utekelezaji wa Programu ya Integrated Training for Entrepreneurship Promotion (INTEP) katika kanda 7 (Dar es Salaam, Mashariki, Kaskazini, Ziwa, Kusini Magharibi, Magharibi na Kati) ambapo jumla ya wanufaika 2,101 (wanawake 1,483) sawa na asilimia 105 ya lengo walipatiwa mafunzo katika fani za ushonaji, kilimo, uvuvi, mama lishe, mapishi na ufugaji kupitia VETA.

**28.** Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha mafunzo kwa vitendo kupitia utaratibu wa uanagenzi kwa wanafunzi wa vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa kuwajengea uwezo walimu 16 na walezi 19 kuhusu utekelezaji wa mafunzo ya uanagenzi pacha. Aidha, imetoa mafunzo kwa wanafunzi 376 ambapo Programu ya Mafunzo ya Uanagenzi 195 (wanawake 87) na programu ya kukuza ajira na ujuzi kwa vijana 181 katika fani za umeme wa viwandani na nishati ya jua, ufundi vipuri, ufundi majokofu, na utayarishaji wa vyakula.

**c. Kuwezesha Ongezeko la Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu**

**29.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha ujenzi wa shule mpya za sekondari ngazi ya kata 228 na shule 26 za Sayansi za Wasichana za bweni za mikoa. Vilevile, imewezesha ujenzi wa shule mpya za msingi 302 nchi nzima;

(ii) imewezesha ujenzi wa madarasa 4,140, maabara 18, mabweni 119, matundu ya vyoo 21,237 na nyumba za walimu 285 zenye uwezo wa kuchukua watumishi 456 katika shule za msingi na sekondari; na

(iii) imewezesha ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa 869, maabara za sayansi 132 na matundu ya vyoo 1,650 katika shule mbalimbali nchini.

**30.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za elimu kwa kutoa ithibati kwa shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imesajili jumla ya shule 1,073 zilizoomba usajili na kukidhi vigezo ambapo; Shule za Awali Pekee 42 (zisizo za Serikali), Awali na Msingi 707 (zisizo za Serikali 187), na Sekondari 324 (zisizo za Serikali 26); na

(ii) imetoa vibali vya kuanzisha shule 251 mpya zilizokidhi vigezo kati ya shule 315 zilizoomba. Kati ya shule hizo, shule za awali pekee 31, awali na msingi 180 na sekondari 40.

**31.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ubora wa elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imefanya tathmini ya jumla ya asasi 7,418 zikiwemo asasi za Serikali 6,011 na zisizo za Serikali 1,407. Katika tathmini hiyo asasi zilizobainika kuwa na mapungufu zilipewa ushauri wa kitaalam na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji; na

(ii) imefanya ufuatiliaji wa ushauri uliotolewa wakati wa tathmini ya jumla katika shule za msingi 1,750, sekondari 382 na chuo cha ualimu kimoja. Ufuatiliaji ulibaini mabadiliko chanya ya viwango vya ubora baada ya kufanyia kazi maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika tathmini ya jumla.

**32.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha fursa ya elimu ya ualimu kwa kusajili jumla ya wanachuo 23,331 (wanawake 11,224) ambapo katika vyuo vya ualimu vya Serikali wanachuo ni 23,162 na Visivyo vya Serikali wanachuo ni 169. Vilevile, imeendelea na ujenzi mpya wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga, Mhonda, Dakawa na Ngorongoro ambapo ujenzi wa vyuo hivyo umefikia asilimia 95.

**33.** Mheshimiwa Spika, umahiri wa walimu na wakufunzi ni nyenzo muhimu katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa walimu wa elimu ya awali 4,000 kuhusu ujuzi wa kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia zinazotokana na rasilimali zinazopatikana katika maeneo yao;

(ii) imetoa mafunzo kwa walezi na waangalizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum 148 kuhusu namna ya kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na stadi za maisha ikiwemo ufugaji wa kuku na uanzishaji wa bustani ili waweze kujikimu.

(iii) imetoa mafunzo kwa walimu 80 wa shule za msingi na sekondari wasioona kuhusu namna ya kutumia vifaa vya kidijiti kama vile kompyuta katika kufundishia na kujifunzia; na

(iv) imetoa mafunzo ya ubainishaji wa watoto wenye mahitaji maalum kwa washiriki 114 wakiwemo maafisa elimu wilaya na mikoa, maafisa ustawi wa jamii, maafisa wauguzi, maafisa taaluma wa mikoa, walimu wa elimu maalum, na maafisa elimu maalum wilaya katika mikoa mitano ambayo ni Tabora, Kigoma, Katavi, Kagera na Rukwa iliyokuwa chini ya wastani wa asilimia 50 ya uandikishaji wa watoto wenye mahitaji maalum.

**34.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha upatikanaji wa vitabu kwa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi, na sekondari ili kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa moduli 12 za mafunzo kwa darasa la awali, I, na III kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa watekelezaji wa mitaala mpya;

(ii) imeandaa mitaala nane na mihtasari 114 katika ngazi ya elimu ya awali, msingi (darasa I - VI), sekondari (kidato cha 1 - 4 na kidato cha 5 - 6) na ualimu (elimu ya Awali, msingi, elimu maalum na mafunzo ya ualimu wa karakana);

(iii) imekamilisha kutafsiri mihtasari 23 ya elimu ya ualimu na aina 93 za vitabu vya mitaala iliyoboreshwa wa darasa la elimu ya awali, darasa la I na III, na kidato cha kwanza mkondo wa amali;

(iv) imeandaa aina 19 ya vitabu vya darasa la awali, I na III katika maandishi makubwa kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na aina 19 nyingine katika maandishi ya breli kwa ajili ya wanafunzi wasioona na aina 31 za vitabu vya kiada kwa kidato cha 5 na 6;

(v) imetoa ithibati ya aina 22 za vitabu vya ziada vya mitaala iliyoboreshwa, mtaala unaoendelea vitabu 156 na maudhui 18 ya kielektroniki;

(vi) imetoa ithibati kwa miswada ya vitabu 162 kati ya 203 kutoka kwa wachapaji binafsi; na

(vii) imechapa na kusambaza vitabu vya kiada nakala 2,687,860 vya sekondari vya masomo ya sayansi na hisabati kidato cha 1 - 4; nakala 4,776,461 za vitabu vya darasa la IV - VII; na nakala 4,000,000 za vitabu vya hadithi kwa elimu ya awali, darasa I na II, 6,060 za vitabu vya breli kwa ajili ya wanafunzi wa awali. Aidha, vitabu vyote vilivyochapwa na kusambazwa vinapatikana pia katika maktaba mtandao ambapo wanafunzi na walimu wanaweza kuvipata bila gharama yoyote ya kuunganishwa kwa mtandao (Zero - Rating) na hivyo kurahisisha upatikanaji wake.

**35.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kukuza ujuzi wa uandishi, kuhamasisha tabia ya usomaji na kuongeza machapisho katika maktaba zetu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imefanya Maadhimisho ya Wiki ya Usomaji Vitabu Mkoani Mwanza ikiwa na kauli mbiu '**Wasomaji na Wachapishaji Tukutane Maktaba'**, lengo ni kuhamasisha jamii kuwa na utamaduni wa kusoma vitabu;

(ii) imeratibu mashindano ya uandishi wa insha kwa wanafunzi 442 wa shule za sekondari ambapo washindi watano walipatikana kwa ajili ya kushiriki mashindano ngazi ya kikanda. Lengo la mashindano hayo ni kukuza stadi na ujuzi wa uandishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini;

(iii) imeratibu utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Unaozingatia Ubunifu uliofanyika tarehe 13 Aprili, 2024 ambapo Mgeni Rasmi katika hafla hiyo alikuwa Prof. Abdulrazak Gurnah ambaye ni mshindi wa Tuzo ya Nobel katika fasihi kwa mwaka 2021. Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Unaozingatia Ubunifu imehusisha mashindano ya uandishi wa riwaya, mashairi na hadithi za watoto ambapo jumla ya miswada 208 (Riwaya 51, Ushairi 97 na Hadithi za watoto 60) ilipokelewa ambapo washindi 10 kutoka katika kila nyanja walitunukiwa cheti kila mmoja. Katika mashindano hayo mshindi wa kwanza alipata ngao pamoja na fedha tasilimu wakati mshindi wa pili na wa tatu walipata zawadi ya fedha tasilimu pekee. Lengo la Tuzo hiyo ni kuhamasisha uandishi utakaosaidia kuongeza idadi ya vitabu vilivyoandikwa na Watanzania na kutumika katika shule zetu badala ya kutegemea vitabu vinavyotoka nje ya nchi; na

(iv) imeendelea kuimarisha fursa za huduma ya maktaba nchini kwa kuendelea na ujenzi wa maktaba ya Kumbukumbu ya John Pombe Magufuli - Chato. Vilevile, imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wakutubi 70 wa maktaba kuhusu huduma za maktaba na matumizi ya mfumo wa malipo ya Serikali. Aidha, imepokea nakala za vitabu 62,777 kutoka katika taasisi mbalimbali za kielimu na kusambaza katika maktaba zetu.

**36.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha fursa na ubora wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum na kuondoa vikwazo katika ufundishaji na ujifunzaji, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha Kiunzi cha Kitaifa cha Kuwezesha Shule zinakuwa Jumuishi zaidi (National Framework for Enabling Schools to Become More Inclusive). Kiunzi hicho kimebainisha vigezo vya shule kuwa jumuishi na namna ya kuvifikia vigezo hivyo;

(ii) imesambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vifaa saidizi kwa ajili ya wanafunzi, wakufunzi, walimu na walimu tarajali wenye mahitaji maalum katika shule za msingi 732, vitengo 565 na shule jumuishi za sekondari 72. Vifaa hivyo ni pamoja na: Hansonet 60, Shimesikio 79, fimbo nyeupe 62, Orbit Reader 107, miwani za jua 52, magongo 29, mashine za breli zinazotumia umeme 17, vitimwendo 120, vioo-kuza vinavyotumia umeme (Electronic Magnifier) 25, kofia 43, karatasi za kuandikia maandishi ya breli box 119 na seika 89 kwa walimu wasioona kwa lengo la kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa elimu maalum; na

(iii) imewezesha zoezi la upimaji kwa wanafunzi 935 viziwi na kubaini wanafunzi 281 wenye usikivu hafifu ambao walipatiwa hearing aids, wanafunzi 300 wenye maambukizi walishauriwa kwenda hospitali na wanafunzi 354 viziwi kabisa walipewa tablets zenye kamusi ya lugha ya alama.

**37.** Mheshimiwa Spika, katika eneo la upimaji na tathmini ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) wa mwaka 2023 kwa wanafunzi **1,545,330** ambao ni sawa na asilimia **91.25** ya wanafunzi **1,693,444** waliosajiliwa. Katika upimaji huo wanafunzi **1,287,934** sawa na asilimia **83.34** walifaulu;

(ii) imeendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi wa mwaka 2023 kwa watahiniwa **1,356,392** ambao ni sawa na asilimia **97.07** kati ya **1,397,293** waliosajiliwa. Katika mtihani huo wanafunzi **1,092,960** sawa na asilimia **80.58** walifaulu;

(iii) imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili wa mwaka 2023 kwa wanafunzi **695,639** ambao ni sawa na asilimia **91.56** kati ya **759,799** waliosajiliwa. Katika upimaji huo wanafunzi **592,741** sawa na asilimia **85.31** walifaulu;

(iv) imeendesha Mtihani wa Kidato cha Nne wa mwaka 2023 kwa watahiniwa **529,596** ambao ni sawa na asilimia **97.47** kati ya **543,332** waliosajiliwa. Katika mtihani huo wanafunzi **471,427** sawa na asilimia **89.36** walifaulu;

(v) imeendesha Mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa **8,630** kati ya watahiniwa **10,953** waliosajiliwa kufanya mtihani ambapo watahiniwa **4,239** sawa na asilimia **49.12** walifaulu; na

(vi) imesajili watahiniwa **104,172** kwa ajili ya Mtihani wa Kidato cha Sita ambao umeanza kufanyika tarehe **6 Mei, 2024** na watahiniwa **11,534** wa Mtihani wa Ualimu.

**38.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha elimu inayotolewa katika vituo vinavyotoa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imesajili wanafunzi 22,131 wakiwemo wasichana 2,794 wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala katika vituo vya elimu ya Watu Wazima. Vilevile, imetoa mafunzo ya kisomo kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa watu wazima 6,238 katika mikoa 26;

(ii) imekamilisha moduli 11 za Hatua ya I na II kwa ajili ya vituo 151 vya elimu ya sekondari kwa Njia Mbadala ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika vituo hivyo; na

(iii) imeongeza idadi ya vituo vya elimu ya sekondari kwa njia mbadala kutoka 168 hadi kufikia 190 kwa lengo la kuongeza fursa kwa wanafunzi waliokosa elimu kwa sababu mbalimbali.

**d. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu**

**39.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha fursa za upatikanaji wa elimu ya juu kupitia utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mikopo kwa wanafunzi 229,652 (mwaka wa kwanza 83,640 na wanaoendelea 146,012) yenye jumla ya **Shilingi 786,724,730,000.00**;

(ii) imetoa ufadhili kwa wanafunzi 1,220 kati ya 1,200 waliolengwa (wanafunzi wapya 915 na wanaoendelea 305) wenye jumla ya **Shilingi 6,367,169,632.00** kupitia **SAMIA** Scholarship;

(iii) imetoa mikopo kwa wanafunzi 2,299 wa ngazi ya stashahada yenye jumla ya **Shilingi 6,114,790,500.00;** na

(iv) imekusanya jumla ya **Shilingi 132,731,358,063.47** sawa na asilima 55 ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni **241** kutokana na mikopo iliyoiva.

**40.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ithibati na uthibiti wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu maombi 144,755 ya wanafunzi walioomba kujiunga na elimu ya juu kwa ngazi ya shahada ya kwanza katika vyuo vikuu nchini kwa mwaka wa masomo 2023/24. Kati ya maombi hayo, waombaji 133,617 sawa na asilimia 92 wamedahiliwa katika vyuo mbalimbali nchini;

(ii) imefanya tathmini na kutoa ithibati ya Mitaala 65 kati ya mitaala 289 iliyopokelewa kwa mchanganuo ufuatao: Ngazi ya astashahada 3, stashahada 3, shahada 20, stashahada ya uzamili 2, uzamili 34 na uzamivu 3; na

(iii) imetathmini na kutambua tuzo 2,076 sawa na asilimia 83 ya tuzo 2,515 zilizowasilishwa kutoka vyuo vya elimu ya juu vya nje ya nchi.

**41.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu na kuongeza fursa katika vyuo vikuu na taasisi za sayansi na teknolojia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na taratibu za ujenzi wa miundombinu katika Kampasi 14 za vyuo vikuu ambapo ujenzi katika Chuo Kikuu Ardhi umefikia asilimia 48, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kampasi kuu asilimia 35, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kampasi ya Rukwa asilimia 45 na Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwl. Julius Nyerere kampasi kuu asilimia 15; Aidha, zoezi la kupata wakandarasi katika kampasi zilizobakia linaendelea; na

(ii) inaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika vyuo vikuu ikiwemo kumbi za mihadhara, hosteli za wanafunzi, madarasa na maabara.

**42.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi za sayansi na teknolojia kwa kuwawezesha jumla ya wanafunzi 3,107 (wanafunzi 517 kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na wanafunzi 2,590 kutoka chuo cha Ufundi Arusha) kuhudhuria mafunzo ya vitendo kwenye viwanda, kampuni na taasisi mbalimbali nchini. Vilevile, imetoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 1,966 wa "cluster" ya pili na ya tatu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

**43.** Mheshimiwa Spika, katika kuwajengea uwezo wahadhiri na watumishi waliopo katika taasisi za elimu ya juu, Serikali imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa wanataaluma 396 (umahiri 189 na uzamivu 207) kutoka vyuo vya elimu ya juu wakiwemo wanataaluma 27 kutoka vyuo binafsi. Vilevile, imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 24 (shahada 9, stashahada 14 na astashahada 1). Aidha, imewezesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 1,557.

**44.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na nchi za nje na vyuo vikuu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu ufadhili wa wanafunzi 23 wanaosoma nchini China kupitia programu ya China Scholarship Council. Vilevile, imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi watano wa kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na

(ii) imefadhili wanafunzi 193 katika programu mbalimbali kupitia Jumuiya ya Madola ya Uingereza 9, Chevening UK 17, Hungary 23, Urusi 90, Mauritius 2 na China 52.

**e. Kuimarisha Uwezo wa Nchi Katika Tafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa Lengo la Kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda**

**45.** Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeendelea kuimarisha tafiti kwa lengo la kutumika kutatua changamoto mbalimbali za jamii na kuchangia katika maendeleo ya nchi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea kuratibu miradi 106 ya utafiti na ubunifu kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia - COSTECH ikiwemo miradi 34 ya utafiti na miradi 72 ya ubunifu katika vyuo vikuu, taasisi za maendeleo pamoja na vyuo vya kati vya ufundi ambapo miradi saba imekamilika na kufungwa. Utekelezaji wa miradi hiyo umewezesha upatikanaji wa bidhaa, teknolojia na kampuni changa. Kwa mfano, kampuni nne zimezalishwa na kusajiliwa kutoka katika miradi hiyo ya ubunifu na kuajiri vijana 27;

(ii) imefanya tafiti 638 kupitia taasisi za elimu ya juu katika maeneo ya elimu, afya, mazingira, uongozi, viwanda, TEHAMA, usafirishaji, kilimo, ubunifu, kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia taka zinazozalishwa katika mazingira ya nyumbani, tiba za wanyama, biashara, haki za binadamu, watu wenye mahitaji maalum, matumizi bora ya ardhi, usanifu na ujenzi wa gharama nafuu wa majengo mapya, njia mbadala za uvunaji wa maji ya mvua; na

(iii) imeendelea kusimamia miradi ya tafiti 199 katika maeneo yafuatayo: utatuzi wa migogoro ya ardhi, matumizi bora ya ardhi, usanifu na ujenzi wa gharama nafuu

za majengo mapya, njia mbadala za uvunaji wa maji ya mvua ili kuongeza huduma ya maji katika majiji, ubunifu na matumizi ya maeneo ya wazi katika kuzuia mafuriko, kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia taka zinazozalishwa katika mazingira ya nyumbani na uzalishaji wa chakula kwa kutumia skimu ndogo ndogo za maji katika vijiji vilivyokaribu na mito.

**46.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi pamoja na kuhamasisha ushiriki wa jamii katika sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa andiko mradi la kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Teknolojia (National Technology Park), kuandaa dira ya miaka 15 ya mahitaji ya teknolojia nchini (National Technology Roadmap);

(ii) imeboresha vyuo vya maendeleo ya wananchi 12 ili vitumike katika kuchagiza uibuaji na uendelezaji wa bunifu na teknolojia (Upgrading 12 FDCs into Zonal/Regional Innovation and Technology Support Centers);

(iii) imeandaa andiko mradi la kuanzisha vituo vinne vya umahiri wa utafiti na ubunifu katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. Aidha, vituo hivyo vitajikita katika Teknolojia zinazoibukia (Emerging Technologies); Bidhaa na Maarifa Asilia (Natural Products and Indigenous Knowledge); Sayansi na Teknolojia za Anga (Space Science and Technologies); Chanjo na Teknolojia za kubaini magonjwa ya binadamu na wanyama (Vaccine and Diagnostics for Human and Animal Diseases); na Teknolojia za kufundishia na kujifunzia yaani (Educational Technologies); na

(iv) imetoa tuzo za watafiti kwa washindi 47 waliochapisha matokeo ya tafiti katika majarida yenye hadhi ya juu kimataifa.

**47.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia taasisi za elimu ya juu imetoa machapisho 1,519 kati ya machapisho 1,806 yaliyolengwa katika majarida mbalimbali ya kitaaluma kwenye ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa lengo la kuongeza maarifa katika jamii kuhusu utatuzi wa changamoto mbalimbali na kuvitangaza vyuo. Vilevile, imefadhili wanataaluma 173 ili kufikia hatua ya kuchapisha machapisho katika majarida mbalimbali.

**48.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya TEHAMA na teknolojia nyingine za kufundishia na kujifunzia kwa lengo kuongeza ufanisi katika ufundishaji;

(ii) imeendelea kusimamia bunifu mbalimbali zilizobuniwa kupitia watumishi na wanafunzi ili ziweze kufika hatua ya kuuzika sokoni, bunifu hizo ni uundaji wa mita za malipo kabla ya matumizi; Programu ya Bi - Shamba na Programu ya Leo Leo Gulio;

(iii) imewezesha taasisi iitwayo **UjuziNet** kutengeneza programu ya simu kwa ajili ya kutafuta taarifa za teknolojia. Programu hiyo itaziwezesha taasisi za umma na binafsi kukusanya taarifa kuhusu Teknolojia zinazopatikana katika sekta mbalimbali. Programu hii imeundwa mahsusi ili kunasa taarifa katika umwagiliaji wa kilimo, taarifa za teknolojia ya afya, na mitambo ya kilimo, kulingana na mahitaji yaliyopokelewa; na

(iv) imewezesha ubiasharishwaji wa bunifu nne (ushonaji, ubunifu wa mavazi, mashine za kuongeza madini joto kwenye chumvi na mashine ya kufungasha bidhaa mbalimbali) katika Kanda ya Dar es Salaam kupitia VETA.

49. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia taasisi za elimu ya juu imeendelea kuimarisha huduma za jamii na kutatua changamoto mbalimbali, kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa ushauri wa kitaalamu katika usanifu na usimamizi wa ujenzi wa ghorofa tatu wa jengo la ofisi za Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba - TMDA Dodoma; usanifu na usimamizi wa ujenzi wa uwanja wa mashujaa (National Heroes Stadium) katika mji wa Serikali Dodoma; usanifu na usimamizi wa ukarabati wa majengo ya biashara, nyumba ya ukewezaji, maisha house, NIC Kisutu, NIC Morogoro na Kihonda apartments. usanifu na usimamizi wa ujenzi wa karakana za TEMESA katika mji wa Dodoma na Geita kupitia VETA; na

(ii) imetoa ushauri kwa wadau mbalimbali ikiwemo huduma za ugani kwa washiriki wapatao 65,306 wakiwemo wakulima, wafugaji, maafisa ugani, watafiti katika nyanja ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na uimara wa udongo.

**50.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha udhibiti na kukuza matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imesajili vituo vipya 43 vya Mionzi ayonishi na kufikisha jumla ya vituo vya mionzi 1,386 vilivyosajiliwa na vituo vipya 42 vya mionzi isiyoayonishi na kufikisha jumla ya vituo vya mionzi isiyoayonishi 409 vilivyosajiliwa. Aidha, imesajili vyanzo vipya 36 vya mionzi na kufikia jumla ya vyanzo vya mionzi 1,647 vilivyosajiliwa;

(ii) imetoa leseni 633 za kumiliki na kutumia vyanzo vya mionzi, uingizaji nchini wa vyanzo vya mionzi 95, utoaji nje ya nchi wa vyanzo vya mionzi 13 na safirishaji wa vyanzo vya mionzi ndani ya nchi 47;

(iii) imepima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 1,980 wanaofanya kazi katika vyanzo vya mionzi katika vituo 429. Aidha, viwango vya mfiduo vilivyopokelewa katika miezi mitatu mfululizo vilianzia 0.1 hadi 3.2 millisievert (mSv), ambavyo viko ndani ya ukomo unaokubalika wa udhibiti;

(iv) imepima sampuli 37,717 za vyakula na mbolea, kati ya sampuli hizo 9,062 ziliingia nchini, sampuli 27,774 zilisafirishwa nje ya nchi na sampuli 695 zilikuwa za mbolea na tumbaku na bidhaa nyingine. Upimaji ulibaini kuwa sampuli hizo hazikuwa na madhara yoyote yatokanayo na mionzi; na

(v) imeanzisha ofisi kwenye Bandari ya Fumba Unguja kwa ajili ya usimamizi wa usalama na udhibiti wa vyanzo vya mionzi ayonishi (ionizing radiation) na mionzi siyoayonishi (non ionizing) kwa ajili ya ulinzi wa umma.

**D. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**51.** Mheshimiwa Spika**,** Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO, imesimamia, imeratibu, imefuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikataba 10 ambayo imeridhiwa kimataifa kama ifuatavyo: mkataba wa kulinda nyara za kiutamaduni katika kipindi cha majanga ya kivita; kulinda tamaduni zisizoshikika; ulinzi wa urithi wa asili na kiutamaduni; kukataza, kuzuia uingizwaji, usafirishaji na umiliki haramu wa nyara za urithi wa kiutamaduni; ulinzi na ukuzaji wa vielelezo vya tamaduni anuai; makubaliano ya uingizwaji wa elimu, malighafi za sayansi na utamaduni; kupinga ubaguzi katika elimu; utambuzi wa mafunzo, vyeti na vigezo vingine vya kitaaluma katika ngazi za juu za elimu katika ukanda wa nchi za afrika; kupinga matumizi ya dawa za kuongeza nguvu na mbinu haramu katika michezo; na mkataba wa ardhi oevu muhimu ya kimataifa kama ya makazi ya dubu maji.

**52.** Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini, lengo namba nne (SDG 4) kuhusu elimu bora na usawa inayotoa fursa ya kujiendeleza kwa wote. Aidha, imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa lengo namba tano (SDG 5) kuhusu usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana;

(ii) imewajengea uelewa wadau kwa kutoa mafunzo kuhusu umuhimu wa Tanzania kuridhia Mkataba wa 2001 wa Urithi wa Chini ya Bahari (Underwater Heritage) uliokuwa na lengo la kulinda urithi wa kiutamaduni husuan kumbukizi za binadamu zenye sifa ya kiutamaduni, kihistoria na kiikolojia; na

(iii) imehamasisha matumizi ya mitandao ya UNESCO (ASPNet, UNEVOC, UNITWIN) kwa wanafunzi kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya juu kwa lengo la kubadilishana taarifa za kitaaluma, kuongeza maarifa na utendaji katika maeneo ya umahiri. Aidha, mpaka sasa taasisi 10 zimejiunga na Mtandao wa ASPnet na taasisi nne na vyuo vikuu viwili vimejiunga na mtandao wa UNITWIN/UNESCO Chairs.

**MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 KWA FUNGU 46**

**53.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vitano vyenye lengo la kuongeza ubora wa elimu kwa kuwezesha vijana wa Kitanzania kupata maarifa, ujuzi, kujiamini, kujiajiri na kuajirika. Vilevile, vipaumbele vyenye kujielekeza katika kutegemeza tafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu katika agenda ya maendeleo ya nchi.

**54.** Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/25 ni kama vifuatavyo:

a) kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria na kuandaa miongozo ya utoaji elimu na mafunzo nchini;

b) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (amali na amali sanifu);

c) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya msingi, sekondari na ualimu;

d) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na

e) kuendeleza tafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

**a. Kuendelea na utekelezaji wa Sera na Mitaala, Mapitio ya Sheria na kuandaa Miongozo ya Utoaji Elimu na Mafunzo Nchini**

**55.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na Mitaala kwa ngazi ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu. Aidha, itaendelea na uandaaji wa zana za utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 ambazo ni Miongozo, Mfumo wa Kitaifa wa Tuzo na Sifa Linganifu (Tanzania Qualification Framework – TQF), Sheria na Kanuni, Mfumo wa Mtaala wa Kitaifa na Mfumo wa Tathmini wa Kitaifa katika ngazi ya Elimu ya Msingi, Sekondari, Ualimu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Juu kwa lengo la kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wa Sera.

**56.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na maboresho ya mitaala ya elimu ya amali sanifu na elimu ya juu ili kuwezesha nchi kuandaa rasilimaliwatu yenye ujuzi na maarifa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya mapitio ya mitaala 171, kuandaa mitaala mipya 18, kuanzisha programu za vipaumbele 145 pamoja na matumizi ya mbinu bunifu za ufundishaji katika elimu ya juu. Aidha, itawezesha ziara za kimkakati kwa wafanyakazi wa sekta ya elimu katika nchi zenye uzoefu wa uandaaji wa rasilimaliwatu yenye maarifa na ujuzi wenye kuchangia katika ukuaji wa kati wa uchumi;

(ii) itasasisha na kuandaa mtaala mpya katika taasisi 17 za elimu ya juu; na

(iii) itahakiki mitaala 230 ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Lengo ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi mipango ya nchi, soko la ajira la kitaifa na kimataifa na kuwawezesha wahitimu kujiajiri na kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira.

**57.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 kwa watendaji wa ngazi zote za elimu na mafunzo wakiwemo walimu wa shule za msingi; walimu wa shule za sekondari; wakufunzi wa vyuo vya ualimu; wakufunzi wa vyuo vya ufundi; wakufunzi wa vyuo vya VETA; wakufunzi wa vyuo vya maendeleo ya wananchi; maafisa elimu msingi, maafisa elimu sekondari, wasimamizi wa elimu ngazi ya mkoa; maafisa elimu kata; wathibiti ubora wa shule; na wanataaluma kutoka taasisi za elimu ya juu. Vilevile, itaendelea kutoa mafunzo kazini kwa walimu wa shule za msingi na sekondari kuhusu mitaala iliyoboreshwa.

**58.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 ili iendane na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023. Vilevile, itafanya mapitio ya sharia na miundo ya taasisi mbalimbali ikiwamo; COSTECH, TLSB, NECTA, VETA, TCU, NACTVET, TIE, TEWW na TEA ili ziendane na maboresho ya Sera na Sheria na makubaliano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa. Vilevile, itafanya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa lengo la kuongeza ufasini wake ikiwamo kurahisisha ufunguaji wa mashauri na utekelezaji wake.

**59.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhuisha miongozo mbalimbali ya utoaji elimu na mafunzo nchini ili kuendana na maboresho ya Mitaala na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 kama ifuatavyo:

(i) itakamilisha Mwongozo wa Kuwatambua na Kuwaendeleza Wanafunzi wenye Vipawa na Vipaji; na

(ii) itaandaa Mwongozo wa Elimu Jumuishi wa Ufundishaji na Matumizi ya Teknolojia kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji na matumizi ya teknolojia katika elimu na mafunzo.

**60.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaongeza wigo wa ukusanyaji, uchakataji na utoaji wa takwimu za elimu kwa kuunganisha mifumo yote ya takwimu za elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, elimu ya juu, pamoja na mifumo ya upimaji na tathmini. Maboresho hayo yatahusisha kujumuisha taarifa za shule binafsi zisizo tumia mitaala ya Taifa. Mabadiliko hayo yatawezesha Wizara kuwa na taarifa za kila mwanafunzi, fani na programu zinazotolewa nchini na kuandaa Kitabu cha Taifa cha Takwimu Muhimu za Elimu (Basic Education





Statistics in Tanzania - BEST) ambacho kitakuwa na taarifa za kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya juu. Kazi ya maboresha hayo imeshaanza na inafanywa na wataalamu wa ndani kutoka vyuo vikuu. Aidha, Serikali itaanzisha jukwaa shirikishi la utafiti la wadau wa elimu ambalo litatambua na kuratibu tafiti za kielimu zinazofanyika nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa maamuzi ya kimageuzi na maendeleo katika sekta yanazingatia taarifa, takwimu na tafiti sahihi zenye maslahi kwa sekta na Taifa kwa ujumla.

**61.** Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha tunaimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika agenda ya maendeleo, Serikali itaendelea na mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknolojia ya Mwaka 1996 kwa lengo la kuandaa sera inayoakisi hali ya sasa na ya baadaye ya maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

**b. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali (Ufundi na Ufundi Stadi) katika Shule za Sekondari na Vyuo vya Amali.**

**62.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na sekondari za amali ili kuongeza fursa za mafunzo kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ujenzi wa shule mpya za sekondari za amali za uhandisi 100 kati ya hizo shule 26 zitaanza kupokea wanafunzi kuanzia Januari 2025. Aidha, ujenzi wa shule za amali utapewa kipaumbele katika maeneo ambayo hayana vyuo ya mafunzo ya ufundi stadi;

(ii) itaendelea na ujenzi wa vyuo 65 vya mafunzo ya ufundi stadi, kati ya hivyo 64 ni vya wilaya na kimoja ni cha ngazi ya Mkoa wa Songwe. Vilevile, imeongeza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo 29 vilivyokamilisha ujenzi;

(iii) itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya nyongeza katika vyuo 10 vya mafunzo ya ufundi stadi (Ndolage-Muleba, Ileje, Newala, Ngorongoro, Gorowa - Babati, Urambo, Kasulu, Mabalanga - Kilindi, Nkasi na Kanadi - Bariadi) ili kuviwezesha vyuo hivyo kufikia viwango vya msingi vya utoaji wa mafunzo; na

(iv) itaendelea na ujenzi wa hosteli mbili katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Kampasi ya Karume zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 768 kwa kila hosteli. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500, ukumbi wa mihadhara utakaohudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na itajenga madarasa 12 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300 kwa kila darasa na ofisi 20 za watumishi katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Kampasi ya Kivukoni. Aidha, itaendelea na ujenzi wa jengo la utawala na madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,800 katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Kampasi ya Pemba. Aidha, itaendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

**63.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza fursa za mafunzo ya amali (elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itasajili vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi 150 ambapo vyuo vya elimu ya ufundi ni 100 na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 50, hivyo kuwa na jumla ya vyuo 504 vya elimu ya ufundi na vyuo 885 vya mafunzo ya ufundi stadi. Usajili wa taasisi hizo utawezesha kuongeza fursa na kutoa mafunzo kwa kuzingatia viwango na ubora;

(ii) itadahili wanafunzi 263,718 wa elimu ya ufundi na mafunzo na ufundi stadi ambapo wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi ni 190,518 na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 73,200 sawa na ongezeko la asilimia 23 ikilinganishwa na udahili wa mwaka 2023/24. Udahili unalenga kuongeza rasilimaliwatu yenye ujuzi na uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa;

(iii) itatoa mikopo kwa wanafunzi wa stashahada takribani 10,000 katika fani za kipumbele na zenye uhaba wa wataalam nchini ikiwamo fani sayansi na ufundi; na

(iv) itadahili wanafunzi 2,089 katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro - MVTTC ili kuongeza idadi ya walimu wanaofundisha vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vya ualimu wa mafunzo ya ufundi.

**64.** Mheshimiwa Spika**,** katika kuwajengea umahiri walimu wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na vyuo vya maendeleo ya wananchi, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itatoa mafunzo kwa walimu 1,000 wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kuhusu tathmini ya mitaala ya umahiri ili kuwawezesha walimu kufundisha na kufanya tathmini ya wanafunzi kwa kuzingatia umahiri; na

(ii) kuendelea kuboresha vituo vya umahiri kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa mafunzo wa fani za kipaumbele kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji.

**c. Kuwezesha Ongezeko la Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu**

**65.** Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ujenzi wa shule za sekondari za kata 226, nyumba za walimu 184 wa sekondari na ununuzi wa vifaa vya maabara;

(ii) itawezesha ujenzi wa madarasa 2,018 (msingi 1,221 na sekondari 797); mabweni 114 kwa shule za sekondari; nyumba za walimu 658 (msingi 567 na sekondari 81) matundu ya vyoo 2,848 (msingi 1,514 na sekondari 884), maabara 10 na vituo vya walimu (TRCs) 300 kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, itakamilisha ujenzi vyumba vya madarasa 111 katika shule za msingi 37, matundu ya vyoo, maabara, nyumba za walimu na mabweni katika shule za sekondari 50; na

(iii) itaweka nishati safi ya kupikia ili kuendelea kuhifadhi na kuimarisha mazingira katika vyuo vya ualimu 11 (Nachingwea, Katoke, Kleruu, Tabora, Dakawa, Patandi, Mpwapwa, Sumbawanga, Mhonda, Kasulu na Monduli). Vilevile, itanunua samani kwa ajili ya Chuo cha Ualimu Sumbawanga, Mhonda, Dakawa na Ngorongoro.

**66.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa ithibati kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itasajili shule za msingi na sekondari takribani 772 ambapo awali pekee 30, awali na msingi 475 (zisizo za Serikali 162), sekondari 266 (zisizo za Serikali 57), chuo cha ualimu kimoja cha binafsi; na

(ii) itafanya tathmini kwa shule 100 zilizopewa usajili wa masharti ili kubaini utekelezaji wa masharti ya usajili.

**67.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uthibiti ubora wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na vyuo vya maendeleo ya wananchi, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya tathmini ya jumla katika asasi 6,620 (shule za awali na msingi 4,965, sekondari 1,525, vyuo vya ualimu 66, vyuo vya maendeleo ya wananchi 14, na vituo 50 vya elimu ya watu wazima na mafunzo nje ya mfumo rasmi). Vilevile, itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa lengo la kubaini ubora katika uandikishaji, ufundishaji na ujifunzaji, usimamizi na uongozi na kutoa ushauri kwa walimu wa masomo katika taasisi 1,010;

(ii) itaendelea na ujenzi wa ofisi ya uthibiti ubora wa shule katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na ukarabati wa ofisi nne za uthibiti ubora wa shule katika Halmashauri ya Mpwapwa, Chato, Mpanda, na Halmashauri ya Mji - Ifakara; na

(iii) itanunua samani na vitendea kazi katika ofisi 210 (halmashauri 184 na mikoa 26) za uthibiti ubora wa shule na itanunua magari 3 kwa ajili ya shughuli za uthibiti ubora wa shule katika Halmashauri ya Mlele, Tunduma na Serengeti.

**68.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari kwa lengo la kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi na hivyo kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na kuchochea tabia na utamaduni wa kujisomea kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itachapa na kusambaza nakala za vitabu 2,000,000 vya masomo ya Hisabati na Sayansi kwa kidato cha 1 hadi 4;

(ii) itaandaa vitabu vya kiada kwa darasa la II na IV, sekondari kidato cha 1 na cha 6 na viongozi vya mwalimu. aidha, itaweka maudhui ya elimu ya sekondari katika mfumo wa kidijiti kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wake;

(iii) itachapa na kusambaza vitabu vya kiada kwa darasa la ii na iv, sekondari kidato cha 1 na cha 6 na viongozi vya mwalimu; na

(iv) itachapa na kusambaza vitabu vya kiada katika maandishi yaliyokuzwa na breli kwa darasa la II na IV, sekondari kidato cha 1 na cha 6 na viongozi vya mwalimu kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa watoto wenyemahitaji maalum.

**69.** Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaendelea kukuza ujuzi wa uandishi na kuhamasisha tabia ya usomaji na kuimarisha matumizi ya maktaba katika ngazi zote za elimu kwa kutekeleza yafuatayo: ilevile, Serikali itaendelea kukuza ujuzi wa uandishi na kuhamasisha tabia ya usomaji na kuimarisha matumizi ya maktaba kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Huduma za Maktaba nchini. Vilevile, itaendelea kununua vitabu kwa ajili ya maktaba za mkoa na kuendeleza Maktaba 15 za Jamii;

(ii) itaendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu yenye lengo la kuhamasisha uandishi na usomaji wa vitabu, kutunza historia na utamaduni wa Mtanzania na kuinua sekta ya uchapaji nchini. Tuzo hizo zitatolewa kwa waandishi mahiri wa riwaya, hadithi fupi na ushairi;

(iii) itagharamia uchapaji, kununua na kusambaza katika taasisi za elimu na maktaba vitabu vya washindi wa tuzo hizo. Mafanikio katika azma hii yamelenga kuwezesha sekta ya uchapishaji na uchapaji na kuongeza ari ya kusoma; na

(iv) itaendelea kuratibu na kukuza stadi na ujuzi wa uandishi insha kwa wanafunzi wa elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu nchini katika nyanja za: ujenzi wa taifa, mageuzi ya kimaendeleo, ustahimilivu na maridhiano. Tutaandaa shindano maalum la uandishi wa insha kwa wanafunzi kuchochea uelewa na fikra tunduizi kuhusu **falsafa ya 4Rs ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.** Vilevile, Serikali itaendelea kuratibu shindano la uandishi wa insha kwa Nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kwa wanafunzi 2,000 wa shule za sekondari.

**70.** Mheshimiwa Spika, Serikali itanunua vifaa vya maabara kwa ajili ya shule za sekondari 1,322 na vyuo 13 vya ualimu pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo 35 vya ualimu. Vilevile, itanunua vifaa vya kujifunzia na kemikali kwa ajili ya kufundishia masomo ya sayansi kwa wanafunzi wa elimu kwa njia mbadala kwa hatua ya I na II.

**71.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaimarisha utoaji wa elimu jumuishi kwa wanafunzi na walimu wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo ili kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itafanya tathmini ya awali ya kubaini hali ya usaidizi uliopo na unaohitajika kwa wanafunzi 1,000 na walimu 200 wenye mahitaji maalum kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalam;

(ii) itajenga uelewa kwa jamii na wadau wa elimu kuhusu elimu jumuishi kwa lengo la kuhamasisha uandikishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(iii) itawajengea uwezo maafisa 368 wa elimu maalum msingi na sekondari kuhusu ubainishaji wa awali wa watoto wenye ulemavu kwa lengo la kurahisisha zoezi la upimaji kwa kiwango kinachohitajika; na

(iv) itanunua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vifaa saidizi kwa wakufunzi 105, walimu 103 na walimu tarajali 188 wenye mahitaji maalum ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji.

**72.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanya upimaji na tathimini ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili kwa watahiniwa **1,681,490** na **882,314** mtawalia wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2024;

(ii) itaendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa **1,241,291** wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Septemba, 2024;

(iii) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Nne na Mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa **559,646** wanaotarajiwa kufanya mitihani hiyo mwezi Novemba, 2024;

(iv) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa **114,500** wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2025; na

(v) itaendesha Mtihani wa Cheti na Stashahada ya Ualimu kwa watahiniwa **8,500** wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2025.

**d. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu**

**73.** Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha na kuimarisha huduma ya utoaji na upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wenye sifa na uhitaji, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka 223,201 hadi 252,245;

(ii) itatoa mikopo kwa wanafunzi 84,500 wa mwaka wa kwanza ambapo shahada ya kwanza 80,000, shahada za juu 2,000, wanaosoma nje ya nchi 500 na **SAMIA** Skolashipu 2,000. Aidha, itatoa mikopo kwa wanafunzi 157,745 wanaoendelea na masomo;

(iii) itatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 40 wenye ufaulu wa juu kwenye masomo ya sayansi hususan wanafunzi wa kike waliohitimu Mtihani wa Taifa ya Kidato cha Sita na shahada ya awali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iv) itaendelea kukusanya madeni ya mikopo iliyoiva ya kiasi cha **Shilingi Bilioni 198** kutoka sekta ya umma na kuimarisha makusanyo kutoka sekta binafsi na isiyo rasmi. Aidha, itatafuta wanufaika wapya **40,000** wenye marejesho ya mikopo iliyoiva ikijumuisha wanufaika wapya **5,000** wenye mikopo chechefu kutoka sekta binafsi na isiyo rasmi; na

(v) itaanza kutoa ufadhili kwa ajili ya shahada za juu ikiwemo eneo la fani ya mionzi na nyuklia.

**74.** Mheshimiwa Spika**,** Serikali itaendelea kutoa ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu katika ngazi ya elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kuratibu udahili wa wanafunzi 145,800 wa mwaka wa kwanza wanaotarajiwa kujiunga na programu mbalimbali za masomo katika vyuo vya elimu ya juu; na

(ii) itafanya tathmini ya maombi ya utambuzi wa tuzo 5,000 za wahitimu zilizotolewa katika vyuo vikuu vya nje na kuzitambua zitakazokidhi vigezo.

**75.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya taasisi za elimu ya juu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itajenga miundombinu katika taasisi za elimu ya juu kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu kwa ajili ya Mabadiliko ya Kiuchumi kama ifuatavyo: kumbi 27 za mihadhara; ofisi 302; vyumba 90 vya madarasa na vyumba 17 vya semina. miundombinu hiyo itajengwa katika kampasi 15 za vyuo vikuu katika mikoa ifuatayo: UDSM (Kagera, Lindi na Zanzibar); MUHAS (Kigoma); ARU (Sengerema-Mwanza); SUA (Katavi); Mzumbe (Tanga); MUST (Rukwa); UDOM (Njombe); MoCU - (Shinyanga); IAA (Manyara na Ruvuma); TIA (Singida); IFM (Simiyu). Vilevile, itaendelea na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia Kampasi Kuu Butiama ambapo chuo hicho kitajenga kampasi yake mkoani Tabora; na

(ii) itaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika taasisi za elimu ya juu ikiwemo ujenzi wa maabara, madarasa na hosteli.

**76.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza idadi ya wanataaluma wenye sifa na kuwajengea uwezo watumishi wasio wanataaluma katika taasisi za elimu ya juu ambapo itagharamia mafunzo kwa wanataaluma 308 na watumishi wasio wanataaluma 23 kwa ngazi ya umahiri na shahada ya uzamivu katika fani mbalimbali.

**e. Kuimarisha Uwezo wa Nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili Kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda**

**77.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaweka mazingira wezeshi kwa kuboresha mifumo ya TEHAMA inayounganisha taasisi za maendeleo ya tafiti, taasisi za elimu ya juu na mifumo ya uratibu wa utafiti na ubunifu ili kurahisisha utendaji wa kazi na upatikanaji wa takwimu mbalimbali zinazohusu utafiti, ubunifu na maendeleo. Vilevile, itaunganisha mifumo ya takwimu za elimu na mafunzo nchini kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi elimu ya juu ili kuimarisha utoaji wa taarifa za elimu na mafunzo.

**78.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha taasisi za elimu ya juu na taasisi za kitafiti kuendelea kufanya utafiti wa kimkakati na kuongeza mchango wake katika ajenda ya maendeleo ya Taifa na kuboresha ustawi wa jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaandaa mikakati ya utekelezaji na usambazaji wa matokeo ya utafiti;

(ii) itafanya tafiti 301 katika maeneo ya elimu, sayansi, teknolojia, utawala, ardhi, mazingira, mazao ya kilimo, mifugo, sayansi ya jamii, uongozi, biashara, afya, mifugo, misitu na uvuvi kwa lengo la kuongeza maarifa na kutatua changamoto za jamii;

(iii) itaandaa machapisho 379 ya tafiti katika maeneo ya elimu, ushirika, afya, usimamizi na uendelezaji ardhi, mazingira, makazi na ujenzi, uongozi; na

(iv) itatoa mafunzo kwa watafiti kuhusu uandaaji na uchapaji wa majarida ya kisayansi ya ndani (Local Peer Review Scientific Journals) na viunzi vya uthibiti.

**79.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa tuzo kwa watafiti watakaochapisha tafiti katika majarida yenye hadhi ya juu kimataifa ili kuhamasisha watafiti wa ndani kufanya utafiti na kuchapisha kazi zao katika majarida husika.

**80.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaanzisha programu itakayowawezesha vijana wanaohitimu katika ngazi mbalimbali za elimu kuendeleza mawazo ya ubunifu ili yawe biashara au kampuni changa (Talent Pool Program) kwa ajili ya kujiajiri au kuajiriwa. Aidha, itawawezesha vijana 20 wenye vipaji na wabunifu katika masuala ya uhandisi na teknolojia kupitia programu atamizi.

**81.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha matumizi salama ya mionzi ya nyuklia nchini, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomu itatekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kudhibiti matumizi ya mionzi nchini kwa kukagua vituo 900 ikiwemo hospitali, vituo vya afya, migodi, viwanja vya ndege, na viwanda na majengo yenye mashine za kupima mionzi ili kuhakikisha uwepo wa mazingira salama kwa wagonjwa, wafanyakazi na umma kwa ujumla;

(ii) itapima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,110 wanaofanya kazi katika mazingira ya vyanzo vya mionzi katika hospitali, migodini na viwandani ili kuwalinda dhidi ya madhara yatokanayo na vyanzo vya mionzi sehemu za kazi; na

(iii) itaendelea na upimaji wa sampuli 50,000 za vyakula, mbolea, tumbaku na bidhaa nyingine zinazoingia na kutoka nchini kupitia mipaka ya nchi ikiwemo viwanja vya ndege na bandari pamoja na sampuli za maji ya visima, wasambazaji na wamiliki wa viwanda ili kuwalinda wananchi dhidi ya madhara yatokanayo na mionzi.

**82.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utafiti wa tiba za saratani, Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Kituo cha Utafiti cha Tiba za Saratani (Oncology Research Centre) katika Jiji la Arusha ili kuleta tija na ufanisi katika kukabiliana na tatizo la saratani nchini pamoja na kuimarisha utafiti na uchunguzi kwa kutumia teknolojia ya nyuklia.

**E. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**83.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO, itaendelea kuratibu, kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kuendelea kuiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika vikao na mikutano ya UNESCO kwa lengo la kutetea maslahi ya nchi;

(ii) kuratibu na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa ya UNESCO ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji; na

(iii) kushirikiana na wadau katika kuhamasisha utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**F. SHUKRANI**

**84.** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa QS. Omary Juma Kipanga (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu na kufikia malengo ya wizara. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Profesa Carolyne Ignatius Nombo, Naibu Makatibu Wakuu, Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Franklin Jasson Rwezimula kwa kunipa ushirikiano. Vilevile, ninaomba kutoa shukrani zangu kwa kamishna wa elimu, wakurugenzi, wakuu wa taasisi na watumishi wote kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa juhudi na ufanisi.

**85.** Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, walimu, wanafunzi, na wadau wote wa elimu kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki na mameneja wa shule, vyuo na taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo nchini.

**86.** Mheshimiwa Spika, vilevile, ninawashukuru washirika wa maendeleo na wadau wote wa elimu ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa mipango na miradi ya elimu, sayansi na teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Afrika Kusini, Brazil, Canada, China, Cuba, Ethiopia, Finland, Hangaria, India, Israel, Italia, Japan, Kenya, Korea ya Kusini, Marekani, Mauritius, Misri, Norway, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, Uswisi. Aidha, natambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

**87.** Mheshimiwa Spika, napenda pia kushukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na: Aga Khan Education Services, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Christian Social Services Commission (CSSC), Comprehensive Nuclear–Test - Ban Treaty Organisation (CTBTO), Deutscher Akademischer Austauschdienst (DAAD), Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO), Global Partnership for Education (GPE), Human Development Innovation Fund (HDIF), Inter University Council for East Africa (IUCEA), International Atomic Energy Agency (IAEA), Japan International Cooperation Agency (JICA), Jumuiya ya Madola, Karibu Tanzania Organization (KTO), Korea International Cooperation Agency (KOICA), Plan International, Swedish International Development Agency (SIDA), Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Umoja wa Nchi za Ulaya, United Nations Development Programme (UNDP), United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO), United Nations International Children's Emergency Fund (UNICEF), United States Agency for International Development (USAID), na Water Aid.

**G. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25**

**88.** Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,965,330,380,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:

(i) **Shilingi 637,287,706,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 585,225,031,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 52,062,675,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(ii) **Shilingi 1,328,042,674,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 1,033,393,669,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 294,649,005,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**89.** Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,882,154,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni **Shilingi 1,319,040,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 1,563,114,000.00.**

**90.** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara (Fungu 46 na Fungu 18) yenye jumla ya **Shilingi 1,968,212,534,000.00.**

**91.** Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**92.** Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara https://www.moe.go.tz

**93.** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.



# UNDP yajitosa kuyapa ahueni Magereza nchini

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) limesema litalisaidia Jeshi la Magereza nchini kuondokana na changamoto na kuwa kituo cha kutoa mafunzo kwa wafungwa ili wanaporudi uraiani watoe mchango kwa jamii.

Hatua hiyo inakuja baada ya UNDP kusaini makubaliano ya ushirikiano wa jeshi hilo Januari mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Mwakilishi Mkazi wa UNDP nchini, Shigeki Komatsobara, aliyasema hayo mkoani Morogoro baada ya kutembelea Magereza ya Mtego wa Simba, Mkono wa Mara, Wami Vijana linalotoa pia elimu kwa vijana.

Vilevile, alitembelea Gereza la Mahabusu Morogoro na Gereza Kuu la Wanawake Kingolwira yaliyopo mkoani humo.

"Tumeona Magereza zilivyo sasa tupo tayari kukaa nao ili kuweza kutatua changamoto zinazowakabili Jeshi la Magereza katika majukumu yao ya kutoa mafunzo kwa wafungwa ili wakirudi katika jamii nao watoe mchango wao," alisema Mwakilishi huyo wa UNDP.

Alisema moja ya maeneo ambayo ameyaona na kuahidi kuyafanyia kazi ni usafiri wa mahabusu kutoka gerezani kwenda mahakamani kutokana na uchakavu wa magari yanayotumika.

Komatsobara alishauri kutumia teknolojia ya mawasiliano ya video ya baadhi ya mahabusu mashauri yao kusikilizwa wakiwa mahabusu na ili kukabiliana na tatizo la msongamano.

Mratibu Mshauri na Utawala Bora wa UNDP, Godfrey Malisa, alisema wametembelea magereza hayo kuona mazingira wanayoishi wafungwa na changamoto linazopitia jeshi hilo katika utekelezaji wa shughuli zake.

Alisema baada ya kujionea changamoto hizo, UNDP na Magereza watakaa chini kutengeneza mradi mkubwa wa kumaliza matatizo hayo na kuwapelekea wadau wengine kwa ajili ya kusaidia wafungwa na watumishi wa jeshi hilo.

Mkuu wa Magereza nchini, Kamishna Jenerali Mzee Ramadhani Nyamka, alisema UNDP wametimiza ahadi yao ya kutembelea magereza ili kuangalia changamoto na kuzipatia ufumbuzi baada ya kuingia makubaliano mapema mwaka huu.

Kuhusu matumizi ya mashauri kutumia teknolojia ya video, alisema Magereza makuu nchini yameanza kutumia teknolojia hiyo na UNDP imeahidi kuongeza nguvu katika eneo hilo.




Meneja Bidhaa na Mauzo wa Benki ya NBC, Dorothea Mabonye (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa huduma ya mpya kwa ajili ya wastaafu inayofahamika kama "Akaunti ya Wastaafu", jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita, yenye lengo la kutoa vipaumbele kwa wastaafu. Wengine ni Mkuu wa Idara ya Wateja wadogo na wakubwa wa NBC, Elibariki Masuke (kulia) na Meneja wa NBC Kanda ya Pwani, Zubeider Haroun. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwanafunzi afa, akutwa amejinyonga uwanjani shuleni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWANAFUNZI wa darasa la tatu wa Shule ya Msingi Lungwa iliyoko Kijiji cha Utengule Kata ya Utengule Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani hapa, Prince Mtivike (9), amefariki dunia baada ya kudaiwa kujinyonga kwa kamba ya viatu pembezoni mwa uwanja wa mpira shuleni hapo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, aliwaambia waandishi wa habari kuwa tukio hilo lilitokea Mei 2 majira ya mchana.

Banga alisema kuwa Prince alikutwa akiwa amejinyonga muda mfupi baada ya kula chakula cha mchana na wanafunzi wenzake shuleni hapo.

Mkuu wa Shule hiyo, Erick Nyongole alilithibitishia Nipashe mwanafunzi huyo kukutwa akiwa amekufa kwa kujinyonga pembezoni mwa uwanja huo.

Nyongole, alisema alipata taarifa kutoka kwa wanafunzi waliokuwa wakicheza na Prince kuwa mwenzao huyo amekufa kujinyonga pembezoni mwa uwanja huo.

Baba mkubwa wa mtoto huyo, Alex Mtivike, alisema taarifa za kifo cha mtoto wao walizipata wakiwa mjini Makambako kutoka kwa baba yake mzazi.

Alisema mtoto wao huyo alikuwa na tabia ya kutoroka nyumbani na kukaa mtaani hata kwa siku tatu na kurudi kwao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Utengule, Antony Myava na Mwenyekiti wa Kamati ya Shule hiyo, Evaristo Mwinami waliwataka wazazi kuwa karibu na watoto wao ili kujua changamoto zinazowakabili.

Baadhi ya wakazi wa Utengule, walielezea kusikitishwa na tukio la mwanafunzi huyo kujinyonga na kuahidi kuendelea kuwa karibu na watoto ili kujua changamoto zao ili kudhibiti matukio mabaya likiwamo la kujiua.

# Wanging'ombe yapokea mabilioni ya elimu

**Na Mwandishi Wetu,**
WANGING'OMBE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe imepokea zaidi ya Sh. bilioni 1.03 kwa ajili ya elimu bila malipo kwa shule 120 .

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Agnetha Mpangile wakati akifungua kikao cha baraza la madiwani cha kipindi cha robo ya tatu kilichofanyika mjini hapa.

Mpangile, alisema halmashauri hiyo kupitia mapato ya ndani, imeendelea kuchangia ujenzi na ukalimishaji wa miundombinu ya elimu katika miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti huyo aliwasisitiza madiwani na watendaji kuendelea kuwahamasisha wananchi kuchangia nguvu zao katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Nawasisitiza viongozi wa vijiji na kata kusoma mapato na matumizi kwa mujibu wa miongozo iliyopo ili kuweka uwazi wa mapato na matumizi ya fedha zote zilizopokelewa na kutumika kwenye shughuli za maendeleo, ikiwamo utambuzi wa nguvu za wananchi," alisema Mpangile.

Awali Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Peter Nyanja, alisema kati ya halmashauri 184 nchini, Wanging'ombe ni kati ya halmashauri tano bora ambazo zinatumia mfumo wa Nesti.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta, aliwataka watendaji kusimamia miradi ambayo inatekelezwa kwa fedha zinatoka serikali kuu ili iwe na ubora kulingana na thamani halisi ya fedha.

Kitta aliwakumbusha viongozi wilayani hapa kuhakikisha wanatatua kero za wananchi.

Diwani wa Kata ya Wanging'ombe, Geofrey Nyagawa, alisema miradi mingi ya serikali inayopelekwa katika maeneo yao haiwashirikishi wananchi.

Wakati huo huo; Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, imepokea zaidi ya shilingi bilioni 1 kwa ajili ya uchimbaji visima vya maji na kukamilisha miradi iliyokwama ili kuwezesha wananchi kupata maji ya uhakika na salama.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Jeremiah Maduhu, aliyasema hayo wakati wa kikao cha Jukwaa la Wadau wa Maji lililofanyika mjini hapa.

Maduhu, alisema serikali kupitia bajeti ya mwaka 2024/25 ilielekeza Sh. milioni 300 kutumika katika uchimbaji wa visima na Sh. millioni 700 kukamilisha baadhi ya miradi iliyokwama kabla ya Juni 30, mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Victoria Mwanziva, aliwataka watendaji wa kata na madiwani wa halmashauri hiyo kuunga mkono ajenda ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani kwa kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo yao na kuhakikisha inakamilika kwa wakati.

Mwanziva, alisema jukwaa hilo limeandaliwa madhubuti ili kujadili na kuhoji changamoto zilizopo katika miradi mbalimbali na kuzitatua ili kuwanusuru wananchi kutembea umbali mrefu kufuata maji kwa matumizi ya kila siku.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Wise Mgina, aliwasihi madiwani kuweka usimamizi mzuri ili kupata fedha hizo kwani vijiji zaidi ya 60 vinapata maji na vinakidhi baadhi ya vigezo.





## Watanzania watakiwa kuchangamkia biashara hewa ukaa

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wametakiwa kuchangamkia fursa za biashara ya hewa ya ukaa kutokana na kuwa na faida nyingi ikiwamo kupata fedha nyingi.

Rai hiyo imetolewa jana na Meneja Mpango wa CookFund wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF), Emmanuel Muro, wakati wa mjadala uliohusu matumizi ya nishati safi ya kupikia, biashara ya hewa ukaa.

Muro alisema: "Ni fursa kwa Watanzania kuanza kushiriki katika biashara ya hewa ya ukaa. Biashara hii siyo kwamba unaanza leo na kuvuna kesho, ni lazima uwe na subira na uvumilivu, misitu tunayo, uzalishaji wa hewa upo, wanunuzi wapo nje ya nchi. Ni suala la kujua nani nimfuate, nani nimshirikishe".

Alisema UNCDF kupitia mpango wa nishati safi ya kupikia linaunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan wa matumizi ya nishati safi.

Alisema Tanzania ina takribani hekta milioni 48.1 za rasilimali za misitu, sawa na asilimia 55 ya ardhi yote ya Tanzania Bara ambayo ikitumika vizuri kupitia miradi ya biashara ya kaboni ni suluhisho muhimu la kupunguza kasi ya uharibifu na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema fursa hiyo kubwa pamoja na fursa nyingine kama vile ardhi oevu vinaweza kutoa faida zaidi katika ufadhili wa kaboni kwa wawekezaji wa ndani.

Mhifadhi wa uoto wa asili kutoka NCMC, Dk. Paul Lyimo, alisema jamii kubwa ya Watanzania inatumia kuni na mkaa katika kupikia.

Alisema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, kaya milioni 13.9 Tanzania wanatumia kuni na mkaa katika kupikia.

Alisema: "Tanzania kuna fursa zaidi ya matumizi ya hewa ya ukaa kwa sababu nusu ya nchi imejaa misitu. Tunapaswa kujielekeza katika biashara ya hewa ya ukaa".

# Vyama vyamvaa Tundu Lissu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BAADHI ya vyama vya siasa vimelaani kauli iliyotolewa na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHAHEMA), Tundu lissu, kwenye majukwaa kuwa ni za kebehi, chuki na kuidhihaki serikali na viongozi wake.

Akizungumza jana na waandishi wa habari visiwani Zanzibar, Mwakilikishi wa mwavuli wa vyama 11 vya siasa, Juma Ali Khatib alisema kiongozi huyo hana nia njema kwa Watanzania kutokana na kuhubiri kauli za kibaguzi hasa kwa upande wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema Watanzania wana maadili yao, wakiongozwa na mila, silka na utamaduni katika misingi ya kuheshimiana na ndiyo sifa ya Mtanzania.

Juma ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha ADA Tadea, alisema asili ya Tanzania linatokana na muunganiko wa wananchi wa pande mbili zilizokuwa huru pamoja na undugu wa damu wa mataifa mawili, hivyo siyo vyema kiongozi huyo kukebehi upande mmoja wa muungano huo. Aidha, alisema Watanzania wamejengwa na misingi ya uhuru katika nchi yao pasipo na mipaka, Mzanzibar kufanya kazi Tanzania Bara au Mtanzania Bara kufanya kazi Zanzibar hakuna kosa kisheria.

Hivyo, alimtaka Msajili wa Vyama vya Siasa nchini achukuwe hatua kwa mujibu wa sheria za vyama na vyombo vya ulinzi na usalama dhidi ya mwanasiasa huyo ili kuwa fundisho kwa watu wengine.

Alisema lengo la Rais Samia Suluhu Hassan kufungua mikutano ya kisiasa ili viongozi wa vyama vya siasa kuendelea kunadi sera zao siyo kuzungumzia kauli za uchochezi ni kufanya mikutano ya kistaarabu.

Naye Haji Ambari kutoka Chama cha NCCR, alisema wakati huu Tanzania ikifikisha miaka 60 ya muungano siyo vyema kuzungumzia chuki za kuwagawa Watanzania bila ya sababu ya msingi au kwa uroho wa madaraka ya mtu fulani.

Alisema wakati umefika kwa Watanzania kutokukubali kugawanywa na wanasiasa ambao hawana nia njema kwa taifa lao hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kuendelea kuhubiri umoja na ushikamano uliopo.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Anna Mbogo (katikati), akizungumza na wanahabari wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), waliokuwa katika ziara ya kimasomo wilayani humo hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaoishi kando ya hifadhi watakiwa kulinda mazingira

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa** BABATI

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Anna Mbogo, amewataka wananchi wanaoishi katika vijiji vilivyozungukwa na hifadhi za wanyamapori kufanya shughuli rafiki ambazo zitalinda mazingira.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) waliofanya ziara wilayani humo ikiwa ni mwendelezo wa mafunzo ya uhifadhi kupitia mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasi.

Mkurugenzi huyo alisema halmashauri hiyo kwa mwaka inapata mapato yasiopungua Sh. milioni 300 kutokana na utalii unaotokana na hifadhi za wanyamapori.

Alisema vijiji 10 vilivyozunguka Hifadhi ya Wanyamapori ya WMA Burunge wanapata mapato ya zaidi ya Sh. bilioni mbili kutokana na utalii, kwamba fedha hizo hugawanywa kwa shughuli za maendeleo.

Alivitaja ni Mwada, Sangaiwe, Ngolley, Vilima Vitatu, Kakoi, Minjingu, Olasiti, Maweni, Magara na Manyara.

Alisema mapato hayo husaidia kufanya maendeleo katika vijiji hivyo ikiwamo ujenzi wa shule kwa ajili ya wanafunzi kuwapunguzia kutembea umbali mrefu.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano wa wadau mbalimbali katika kulinda na kuhifadhi mazingira ikiwamo Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili.

Alisema bila ya kufanya shughuli rafiki za kimazingira katika hifadhi wanyamapori watashindwa kupita katika njia zao za asili kutoka sehemu moja kwenda nyingine na kusababisha kutoweka.

Alisema wanajitahidi sana hifadhi zilizomo wilayani humo ikiwamo Hifadhi ya Tarangile, Burunge na Manyara kuleta manufaa kwa wananchi na serikali kupata kipato kwa sababu kama wanyama watatoweka hakuna mtalii atakayefika hivyo serikali na wananchi kukosa mapato.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Faraja Ngerageza, alisema waandishi wa habari wananafasi kubwa kutangaza fursa zilizopo katika kutangaza utalii ili serikali kuendelea kupata kipato kwa kupata watalii wengi.

Alisema uhifadhi wa wanyamapori na mazingira unafaida nyingi ikiwamo kuchangia mapato ya nchi, kukuza biashara katika mkoa huo ambapo kuna wawekezaji wengi wa hoteli na uwepo wa shughuli nyingi za kukuza kipato kwa wananchi.

Ofisa Wanyamapori mkoani humo, Fred Mwasengo, alisema wanatarajia kutangaza maeneo ya uhifadhi wa ushoroba ambayo hayatoruhusiwa kufanywa shughuli zisizorafiki ambazo zinakwenda kinyume na uhifadhi wa mazingira na wala wananchi hawatonyang'anywa ardhi yao.

Ofisa Misitu na Mazingira mkoani humo, Michael Gwandu, alisema ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi ni muhimu katika kufaidika na rasilimali zilizopo.

# Kamati yashauri bajeti ya elimu

**Na Romana Mallya**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo imekosoa bajeti iliyotengwa na serikali katika sekta ya elimu kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Aidha, imeishauri kuendelea kuongeza bajeti ya wizara hiyo, ili kuboresha na kuimarisha sekta ya elimu na kukuza maendeleo ya taifa.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda jana aliomba Bunge liidhinishe makadirio ya Sh. trilioni 1.96 kwa ajili ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Husna Sekiboko, akiwasilisha maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo, alisema kamati haijaridhishwa na wizara ilivyotenga kwenye bajeti ya elimu, mikopo elimu ya juu na upungufu wa fedha za kuchapisha vitabu.

Alisema kamati ilipochambua makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ilibaini kuwa makadirio yameongezeka kwa asilimia 68.

"Matokeo hayo ya uchambuzi yanaonyesha kuwa serikali imeongeza kipaumbele katika miradi inayotekelezwa na wizara hii. Pamoja na ongezeko hilo, bado bajeti ya elimu ni asilimia 14 tu ya bajeti yote ya serikali, hivyo kutokufikia lengo la kimataifa la asilimia 20 ya bajeti yote ya serikali," alisema.

Pamoja na ongezeko hilo, alisema bado kamati haikuridhishwa na fedha zilizotengwa katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 na Mitaala ya Elimu ambapo utasababisha upungufu wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia,

Pia alisema utasababisha upungufu wa walimu wenye ubora na sifa kulingana na mitaala mipya na hata kuathiri uwezo wa wanafunzi kufikia mafanikio ya elimu.

**MIKOPO ELIMU JUU**

Alisema kamati imebaini fedha zilizotengwa kwa ajili ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) zimepungua ukilinganisha na mwaka 2023/2024, zinaweza kusababisha upungufu wa wanafunzi wengi wenye uhitaji kukosa fursa za elimu ya juu na wenye uwezo mdogo wa kifedha.

Alisema kamati imebaini bajeti hiyo sehemu kubwa ni bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambayo ni asilimia 60.33 ya bajeti ya maendeleo.

"Hali hii inakwamisha dhamira ya kuimarisha miundombinu na taratibu za nchi kupata Watanzania walioelimika na wanaoendelea kujielimisha na kuongeza tija katika maendeleo ya taifa.

"Kamati inaishauri serikali kuendelea kuongeza bajeti ya wizara hii, ili kuboresha na kuimarisha Sekta ya Elimu na kukuza maendeleo ya taifa," alisema.

**UCHAPISHAJI VITABU**

Alisema kamati imebaini upungufu wa fedha za kuchapisha vitabu Taasisi ya Elimu Tanzania ambapo kwa sasa uwiano wa vitabu katika shule za awali, msingi kwa mwanafunzi ni 1:5 na mahitaji ni 1:3.

Pia alisema kamati imebaini kuwa, Sh. bilioni 17 zilizopelekwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) tangu mwezi Novemba, 2023, zilikaa hadi mwezi Machi 2024, takribani miezi 5 bila kutumika na kusababisha kurejeshwa Hazina, ingawa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ilikuwa inazihitaji kwa ajili ya uchapishaji vitabu.

Kutokana na hali hiyo, alisema kamati inaishauri serikali kuwa, kwa kuwa jukumu la kuandika, kuchapa na kusambaza vitabu linatekelezwa na Wizara kupitia TET, ni vema fedha za uchapishaji wa vitabu zipelekwe TET moja kwa moja kupitia wizara, ili kuongeza ufanisi, kasi na kufikia malengo ya wizara katika uandaaji na usambazaji wa vitabu shuleni.

Kadhalika, alisema kamati inaishauri serikali kuhakikisha walimu wote wanapaswa siyo tu kuufahamu vizuri mitaala mipya, lakini pia kujengewa uwezo wa mafunzo ya namna bora ya utekelezaji.

Kamati ilisema lengo ni ili waweze kuboresha ujuzi na kupata mbinu mbalimbali za ufundishaji ambazo zitasaidia kujifunza maarifa mapya.

Pia alisema kamati ilishauri mafunzo hayo yatolewe kwa walimu wote nchini wa shule za msingi na sekondari.

"Kamati inashauri waraka uliotolewa na Rais (Re-entry) wa kuwarudisha wanafunzi wa kike waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali, uingizwe katika marekebisho ya Sheria ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwa sheria iliyoko sasa haina kipengele hicho," alisema.

**VETA**

Kamati hiyo imetaka maboresho yafanyike Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) iongezewe bajeti kwa ajili ya uendeshaji wa vyuo vipya 29 vilivyoongezeka ili viweze kutoa mafunzo na kuleta tija iliyokusudiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kuwezesha Watanzania hususan vijana kupata ujuzi utakaowawezesha kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kujiajiri.

Pia imeshauri wizara iweke mpango madhubuti kwa ajili ya uendeshaji wa vyuo vinavyoendelea kujengwa ambapo vikikamilika taasisi hiyo itakuwa na jumla ya vyuo 145 kutoka 51 vilivyokuwapo hapo awali.

"Kamati inaishauri serikali kuwa, vifungu vya fedha za nje vinavyotekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia vitanuliwe bila kuathiri Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi ya fedha za Serikali ili zitekeleze miradi iliyokusudiwa," alisema.

Aidha, kamati hiyo imebaini kuwapo kwa ongezeko kubwa la mdondoko wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari hususan watoto wa kiume, hali inayochangia ongezeko kubwa la watoto wa kiume kuwapo mtaani kunakochangiwa na kutokuwapo kwa mkazo wa masomo kwa kundi hilo.

"Serikali iweke mkakati madhubiti wa kuhakikisha wanafunzi wote walioandikishwa shule wanahitimu masomo yao.

"Aidha, waraka uliotumika kuwarudisha watoto wa kike shuleni utumike pia, kuwarudisha watoto wa kiume shuleni. Vilevile walimu wapewe mafunzo ya kufundisha watoto waliopo nje ya mfumo rasmi," alisema.

## Serikali yataka kamati DNA kuzingatia maadili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeagiza Kamati ya Kitaalamu ya Vinasaba vya Binadamu (DNA) kuzingatia masuala ya kimaadili na mabadiliko ya teknolojia kwenye uchunguzi wa vinasaba, ili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza kijamii na kiusalama.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, aliyasema hayo juzi kwenye uzinduzi wa kamati hiyo jijini hapa.

Alisema serikali ina imani na kamati hiyo kwa kuwa itasaidia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kutimiza wajibu wake hasa ikizingatiwa kwa sasa kuna kukua kwa teknolojia ulimwenguni.

"Hili ni eneo nyeti sana kuna uhalifu mwingi kupitia vinasaba, mtu akiiba DNA anatumia kama utambulisho kwenda kufanya uhalifu sehemu nyingine. Haya ni mambo nyeti tunatakiwa kuwa makini pamoja na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya vizuri hatutakiwi kubweteka.

"Kwa mfano uchunguzi wa vinasaba, kama kuna ubishani huyu mtoto si wa kwangu hiyo kama ikifanyika kiholela na kutumbukia kwenye mikono ambayo si yenyewe inaweza kuleta balaa," alisema.

Alihimiza matumizi ya teknolojia ya uzalishaji wa taarifa za vinasaba kwa manufaa ya nchi kwa kuwa kuna sehemu nyingine zinatumika hata kutengeneza matibabu ya selimundu, saratani.

Kadhalika, alisema vyombo vya ulinzi na usalama katika kazi zao vinahitaji kupata taarifa sahihi, ili ziwasaidia kubaini mhalifu au chombo kilichotumika.

"Kuna teknolojia ya uhariri wa vinasaba inaweza kuleta balaa kwa binadamu hata kubadili kizazi kizima, mjue kazi mliyonayo ni kubwa wanakuja watafiti ndani na nje kwenye eneo hili," alisema.

Alisema kamati hiyo ina jukumu la kusimamia matumizi sahihi ya teknolojia kwenye vinasaba vya masuala ya kibinadamu, vyakula, utatuzi wa migogoro, ubora wa bidhaa na makosa ya jinai.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, alisema uzinduzi wa kamati hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa kifungu cha nane cha Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba vya Binadamu Sura 73 ambayo ni mojawapo ya majukumu makuu ya mamlaka katika kuimarisha utekelezaji wa sheria husika.

Alisema ushauri wa kamati hiyo ni muhimu katika kuendeleza matumizi ya teknolojia ya vinasaba vya binadamu nchini na kusaidia utatuzi wa kero mbalimbali za kijamii.

"Changamoto hizi ni pamoja na uchunguzi wa jinai na kusaidia kupambana na uhalifu, utoaji wa huduma za matibabu ya kibingwa, tafiti za vinasaba, utatuzi wa changamoto za kijamii na utambuzi wa miili isiyotambulika wakati wa majanga," alisema.

Mganga Mkuu wa Serikali na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Prof. Tumaini Nagu, aliahidi kuzingatia maelekezo kutokana na unyeti wa taarifa za vinasaba.

IN THE DISTRICT COURT OF KYELA
AT KYELA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 9119 OF 2024

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE SPAITA ANDENDEKISYE MWAMPUGA

AND

In the matter of Application for Letters of Administration by TUSEKILE GIDION MWALWAJO

GENERAL CITATION (RULE 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 14th day of May, 2024.
Dated at Kyela this 06th day of May, 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA

Notice/Summons to appear (O.V.R.20 (1) of (CPC) (Substituted Service)

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(LAND DIVISION)
AT DAR ES SALAAM

MISC. LAND CASE APPLICATION NO. 5367 OF 2024

MUSHARA INVESTMENT CO LTD..............APPLICANT

VERSUS

PAUL CUTHBERT TULAONA MTWEVE.........RESPONDENT

TO: PAUL CUTHBERT TULAONA MTWEVE

**WHEREAS:** The above-named Defendant has instituted a suit against you; you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent dully authorized on 13th May, 2024 at 9:00 hrs FOR MENTION before Hon. M.R. Gwae, J (Room No. 2) and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence.

**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day before mentioned, the application will be heard and determined in your absence.

Given under my Hand and the seal of this court, this 03rd day of May, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI**

**MAURUS ZEBEDAYO MBOGO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE USAJILI NAMBA **T 793 CDC** AINA YA **BOXER**, KWA YEYOTE ALIETOKEA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAWE
POLISI TAARIFA
**PHQ/IRI/KIL/5762/2024.**

**KUPOTELEWA NA OFA YA KIWANJA**

**HELLEN SYLVESTER MALEZA** ambaye ni Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **Jonam Nelson Maleza.** Anatangaza kupotelewa na Offa ya Kiwanja namba **439 Kitalu D** yenye jina la **Jonam Nelson Maleza** kilichopo **Njiro Mkoani Arusha.** kwa yeyote akaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na **Hellen Sylvester Maleza kwa simu namba 0754-048191**
TAARIFA YA POLISI
**PHQ/ARU/ARU/12610/2024**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**DAVID PETER MLAKI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI** yenye usajili namba **T 352 DLE,** CHASSIS NAMBA: **DA63T215169** na ENGINE NAMBA : **K6A5903748.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/13976/2024**

## HABARI KIMATAIFA

# Mtoto adondokewa na kifusi, afariki

**NAIROBI,** Kenya

MWANAMKE mmoja kutoka Kisumu nchini Kenya anakabiliana na maumivu makali kutokana na msiba wa mtoto wake wa kiume Ian mwenye umri wa miaka 17 aliyeuawa baada ya tingatinga kuvunja nyumba yao akiwa ndani.

Ilielezwa kuwa kifo cha Ian kilitokana na ubomoaji unaoendelea wa nyumba zilizojengwa kwenye maeneo ya ukingoni mwa mito, hatua iliyochochewa na mvua kubwa iliyokuwa ikiendelea kunyesha ambayo ilisababisha vifo vya zaidi ya watu 228.

**Wakapiga kelele wakisema kuwa Ian amefariki dunia wakitaka kusitisha ubomoaji kwa sababu watoto walikuwa bado ndani ya nyumba, lakini wabomoaji na polisi walikataa kusikiliza.**

Katika video iliyonaswa na Eastleigh Voice, mwanamke huyo aliyefadhaika alifichua kwamba Ian amekuwa akipambana na ugonjwa wa seli mundu. Na kwamba wakati akikutwa na umauti, alikuwa ameondoka nyumbani kwenda kumtafutia dawa.

"Ian ni mtoto wangu wa pili, amekuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa 'sickle cell' niliienda kumtafutia dawa, wakati narudi mtoto wa jirani yangu alinijulisha kuwa Ian amekufa, tingatinga zilikuwa zikibomoa nyumba zetu na mwanangu yuko ndani.

"Wakapiga kelele wakisema kuwa Ian amefariki dunia wakitaka kusitisha ubomoaji kwa sababu watoto walikuwa bado ndani ya nyumba, lakini wabomoaji na polisi walikataa kusikiliza," alibainisha.

Aliongeza kuwa jambo lililomzidishia machungu ni baada ya polisi waliokuwepo eneo la tukio kumshauri mhudumu wa tingatinga kumzika mtoto huyo hapo hapo.

Kwa mujibu wa mwanamke huyo, walipinga pendekezo hilo na kuwafanya maofisa hao kutoweka haraka katika eneo la tukio. Katika hali ya kuhuzunisha, maofisa hao waliporudi kuchukua mwili huo, walimnyima fursa ya kuandamana na mwanawe aliyefariki hadi chumba cha kuhifadhia maiti.

Mwanamke huyo alishutumu serikali kwa kuhusika katika kifo cha mwanawe wa pekee, akiomba waachilie mwili wake ili azikwe Kisumu, badala ya Lang'ata.

"Polisi waliona kila kitu wanamzikaje mtoto wa mtu na kukimbia, walipofika kwa ajili ya maiti walikataa niwasindikize, serikali imechukua maisha ya mwanangu, tafadhali serikali mrudisheni mtoto wangu. Natamani kumzika Kisumu. Hawezi kuzikwa Lang'ata kwa sababu sina mtoto wa kiume kama Ian," alisema mwanamke huyo.

Amri ya ubomoaji wa nyumba hizo ilitolewa na Rais William Ruto siku chache zilizopita akilenga kuwaepusha kukutwa ma madhara zaidi ya mafuriko wananchi walioweka makazi yao pembezoni mwa mto. Na kwamba baadhi yao hawakutii agizo la kuhama katika makazi hayo hadi zoezi la ubomoaji lilipowakuta. **KTN**



Rais wa Kenya, William Ruto akiwa na moja ya familia inayoishi katika mazingira magumu katika nyumba za Kanjo huko Mathare, baada ya kufanya ziara ya kushtukiza, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Putin aapishwa kuongoza Russia

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia Vladimir Putin (pichani) ameapishwa na kuanza rasmi muhula mwingine wa miaka mitano madarakani baada ya kupata ushindi wa kishindo wa asilimia 87 ya kura zilizopigwa siku chche zilizopita nchini humo.

Putin mwenye umri wa miaka 71 na ambaye ametawala siasa za Russia kwa miaka 24, amekula kiapo kwenye hafla iliyofanyika katika Ikulu ya Kremlin mjini Moscow, na kuhudhuriwa na wanasiasa waandamizi wa nchini humo, pamoja na wageni waalikwa ambao ni viongozi wenye vyeo vya juu.

Katika hotuba yake baada ya kuapishwa jana, Putin alisema mifumo ya nchi yake ni lazima iwe tayari kukabiliana na kitisho cha aina yoyote lakini akasisitiza kuwa, Russia haitositisha mazungumzo na mataifa ya Magharibi huku akazitaka nchi hizo kuwa na maamuzi.

Ilibainishwa kuwa Putin aliifanyia marekebisho katiba ya Russia miaka michache iliyopita. Mabadiliko hayo yatamuwezesha Putin baada ya muhula wake wa sasa kumalizika mwaka 2030, kuruhusiwa kugombea tena na kusalia madarakani hadi mwaka 2036, atakapokuwa na umri wa miaka 83. **DW**



# Biden aionya Israel kuivamia Rafah

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani Joe Biden amemwonya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, dhidi ya kuuvamia mji wa Rafah unaohifadhi mamilioni ya Wapalestina waliokimbia mapigano kutoka maeneo mengine ya Ukanda wa Gaza.

Katika mazungumzo yaliyofanyika jana kwa njia ya simu kati ya Netanyahu na Rais Biden, alimtaka kiongozi huyo kutoendelea na operesheni yake ya kijeshi ya kuvamia mji huo uliofurika wakimbizi wa ndani.

Matamshi ya Rais Biden yanajiri baada ya amri iliyotolewa na Israel ya kutaka watu wayahame maeneo kadhaa ya mji huo huku vikosi vya Israel vikiongeza mashambulizi ya anga.

Hata hivyo, licha ya tahadhari hiyo, saa chache baada ya mazungumzo ya simu kati ya Biden na Netanyahu, Israel ilirejea tena onyo lake kwa Wapalestina ikiwataka kuondoka Rafah ikisema inajitayarisha kutuma vikosi vyake vya ardhini.

Vile vile, kwa mujibu wa taarifa ya ofisa wa Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) wana udhibiti wa uendeshaji wa upande wa Gaza wa kivuko cha Rafah, huku ikibainishwa kuwa vifaru vya Israel viliingia kwenye eneo hilo, ambalo ni kituo cha kusini kutoka Gaza na mpakani mwa Misri.

Ilibainishwa kuwa wanajeshi wanaendelea kusema kwamba kama sehemu ya operesheni yao, walishambulia na kumaliza malengo ya ugaidi ya Hamas katika eneo la Rafah na kwamba takriban magaidi 20 wameangamizwa na mahandaki matatu yamepatikana.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa IDF itaendelea kufanya operesheni dhidi ya Hamas mashariki mwa Rafah na katika eneo la kivuko cha Rafah.

Waziri Netanyahu alisema pendekezo jipya la usitishaji vita huko Gaza liko mbali na mahitaji ya kimsingi ya Israel lakini mazungumzo yataendelea, maoni aliyotoa baada ya Hamas kusema kuwa imekubali masharti ya mapatano yaliyotolewa na wapatanishi wa Qatar na Misri.

Ofisa katika kundi hilo la Wapalestina alisema mpira sasa uko upande wa Israel, huku ikibainishwa kwamba usiku kucha, vikosi vya Israel na vifaru vilionekana karibu na kivuko cha mpaka cha Rafah kusini mwa Gaza.

Hapo awali, ilibainishwa kuwa Jeshi la Israel lilifanya mashambulizi ya anga katika mji wa Rafah, mpakani na Misri, baada ya kuwaonya Wapalestina kuhama maeneo ya mashariki mwa mji huo.

Makumi ya wakaazi wanaaminika kuathiriwa na operesheni hiyo na wengi walionekana wakining'inia kwenye magari na mikokoteni ya punda juzi.

Israel imetishia kwa muda mrefu mashambulizi dhidi ya Hamas katika mji huo wenye zaidi ya watu milioni 1.4, ambao wengi wao wametafuta hifadhi kutokana na mashambulizi ya Israel katika maeneo mengine ya Gaza. **BBC, DW**

# FEI TOTO AIKARIBIA REKODI MABAO YA BOCCO AZAM FC

Na Adam Fungamwango

LICHA ya mabao yake 15 kumfanya kuongoza kwenye orodha ya Ligi Kuu Tanzania Bara, akisaka Kiatu cha Dhahabu ukiwa msimu wake wa kwanza tangu kujiunga na Azam FC, Feisal Salum, anahitaji kufunga mabao manne ili kuweza kufikia rekodi ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja kwenye timu hiyo, inayoshikiliwa na straika wa zamani wa timu hiyo, John Bocco msimu wa 2011/12.

Feisal, maarufu kama Fei Toto, amekuwa kwenye kiwango cha hali juu msimu huu, ukiwa ni wake wa kwanza akiwa na timu hiyo, akitokea Yanga, ambapo juzi alifunga bao moja na kutoa pasi ya bao na kuiongoza timu yake kushinda 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, mechi ikichezwa, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Kwa sasa amelingana kila kitu na kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, kila moja akiwa na mabao 15, pamoja na 'asisti' saba na kuifanya vita ya kuwania ufungaji bora wa Ligi Kuu msimu huu kuwa mgumu kama ilivyokuwa msimu uliopita ambapo, Fiston Mayele wa Yanga na Saido Ntibazonkiza wa Simba walilingana kila mmoja akipachika mabao 17.

Wakati anapachika mabao kutwaa Kiatu cha Dhahabu, Fei Toto pia anaisaka rekodi iliyowekwa na Bocco, ambaye ndiye mchezaji aliyefunga mabao mengi kwenye klabu ya Azam kwa msimu mmoja mpaka sasa, ambapo 2011/12, alipachika mabao 19 na kuibuka kinara wa upachikaji mabao kwenye Ligi Kuu, hivyo mchezaji huyo anahitaji mabao manne tu katika michezo mitano iliyosalia, huku akihitaji matano kuivunja.

"Kama nilivyoosema siku za nyuma, na nitaendelea kusema kuwa sishindani na mtu, wala kuvunja rekodi ya mtu yeyote, mimi naisaidia timu yangu ya Azam kushinda, hayo mengine yatahesabiwa ligi ikiisha, lakini kwa sasa mimi ninachojua, ni kufunga mabao na kutoa 'asisti' ili timu yangu ishinde," alisema mchezaji huyo anayezicheza pia timu za Zanzibar Heroes na Taifa Stars.

**Mpaka sasa amehusika kwenye jumla ya mabao 22 kati ya 52 ambayo timu yake imefunga.**

Mbali na rekodi hiyo, Fei Toto amebakisha bao moja tu kuweza kumfikia Mrisho Ngassa, aliyepachika mabao 16 akiwa na klabu hiyo, msimu wa 2010/11, akiwa mfungaji bora, pia anahitaji mawili kufikia rekodi ya winga wa zamani wa klabu hiyo, Kipre Tchetche, aliyemaliza na mabao 17 msimu wa 2012/12 na kuibuka mfungaji bora wa Ligi Kuu.

## MWANA FA CUP...




Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Jimbo la Muheza mkoani Tanga, Hamisi Mwinjuma maarufu Mwana FA akisalimiana na wachezaji wa timu ya Ubembe FC na Kisiwani FC kabla ya mchezo wa Ligi ya Mwana FA Cup kuanza katika Uwanja wa Jitegemee wilayani humo mwishoni mwa wiki. Ubembe FC waliibuka na ushindi wa bao 1-0. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# *Timu tano CECAFA kibaruani Afrika*

Na Somoe Ng'itu

TIMU tano za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), zinatarajia kushuka katika viwanja tofauti ili kucheza mechi za raundi ya tatu kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa Wasichama wa umri wa chini ya miaka 17 (U-17 FIFA Women World Cup).

Miamba ya Timu ya Taifa ya Tanzania maarufu Serengeti Girls, ambayo ilishiriki fainali hizo mwaka 2022 huko India na kutolewa katika hatua ya robo fainali, ilishaiaga michuano hiyo kwa kufungwa na yosso wenzao wa Zambia baada ya kukubali kichapo katika mechi zote mbili.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa CECAFA, Auka Gecheo, aliliambia gazeti hili timu zote tano ziko katika hali nzuri na wanaamini ukanda huu unaweza kutoka timu zaidi ya moja katika fainali zijazo za michuano hiyo.

"Tumekuwa na mikakati ya kuimarisha timu za vijana kwa sababu tunaamini ndio watajenga timu imara za wakubwa, kila kitu kinakwenda vema," alisema ofisa huyo.

Ethiopia inatarajia kuwakaribisha Kenya katika mechi itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Abebe Bikila ulioko Adis Ababa na siku mbili baadaye Djibouti watawaalika Burundi kwenye uwanja huo.

Mechi nyingine ya wawakilishi wa CECAFA itakuwa ni kati ya yosso wa Uganda dhidi ya wenyeji wao, Zambia ambayo itachezwa kwenye Uwanja wa Nkoloma.

## Katwila hajakata tamaa Mtibwa

Na Somoe Ng'itu

LICHA ya timu yake kuburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema wataendelea kupambana hadi mechi yao ya kufunga pazia ya msimu na wanaamini huenda mambo yakabadilika.

Mtibwa Sugar sasa inajiandaa kuikaribisha Tabora United, mechi itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Manungu Complex ulioko Turiani, Morogoro.

Katwila aliliambia gazeti hili licha ya kupoteza mechi, wachezaji wake wanajitahidi kupunguza makosa jambo ambalo anaamini wanaweza kujinasua katika janga la kushuka daraja.

"Ni kweli unapopoteza mechi hali inakuwa ngumu, lakini hayo ndio matokeo ya mpira, hatua ambayo tupo hakuna mechi inayotabirika, kila timu inapambana kusaka matokeo mazuri, sisi pia hatujakata tamaa, ni upepo tu bado hauko vizuri upande wetu," Katwila alisema.

"Hatutawadharau Tabora United, kila timu iko katika hali mbaya, tutaingia uwanjani kwa tahadhari, kwa sasa hakuna kusema unacheza nyumbani au ugenini, tuko vitani," aliongeza kocha huyo.

Baada ya juzi kuchapwa mabao 2-0 wakiwa nyumbani, Mtibwa Sugar imeendelea kuburuza mkia ikiwa na pointi 17 wakati mabingwa watetezi, Yanga wakiendelea kujiimarisha kileleni.

## Gofu kwa vijana Jumamosi Lugalo

Na Shufaa Lyimo

MASHINDANO ya vijana ya mchezo wa gofu yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi Jumamosi wiki hii katika viwanja vya Klabu ya Gofu Lugalo jijini Dar es Salaam, imethibitishwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Afisa Habari wa klabu hiyo, Meja Selemani Semunyu, alisema lengo la shindano hilo ni kuchangia timu ya watoto kwa kuthamini mchango wao.

"Tumewekeza nguvu nyingi kuhakikisha program ya vijana inakuwa siku hadi siku, lengo ni kuinua vipaji vyao ambavyo vitaisaidia nchi yetu hapo baadaye," alisema Meja Semunyu.

Aidha, alisema kutokana na ukarabati walioufanya miundombinu ya viwanja ipo vizuri licha ya kuwapo hali ya mvua jijini Dar es Salaam.

Alizitaka klabu zote za gofu hapa nchini na wadau mbalimbali kujitokeza kushiriki shindano hilo ili wawaunge mkono watoto hao.

## ZISIKUPITE

### NUNEZ NA BARCELONA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Uruguay, Darwin Nunez, 24, ameibuka kama lengo kuu la kushtukiza kwa Barcelona, huku mchezaji huyo akionekana kama mbadala wa Robert Lewandowski, 35, wa Poland. ***(Sun)***

### GYOKERES AKATAA HAKIKISHO

MSHAMBULIAJI wa Sweden, Viktor Gyokeres, 25, amekataa kutoa hakikisho la kubakia katika Klabu ya Sporting Lisbon huku Arsenal ikimtaka ***(Standard)***

### SANCHO HATAKI KUREJEA

MSHAMBULIAJI wa England, Jadon Sancho, 24, hataki kurejea Manchester United mwishoni mwa muda wake wa mkopo kutoka Borussia Dortmund. ***(Talksport)***

### CHELSEA KWA SUDAKOV

CHELSEA imezidisha juhudi zao za kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Shakhtar Donetsk raia wa Ukraine mwenye thamani ya pauni milioni 65, Georgiy Sudakov, 21, ambaye pia anafuatiliwa na Arsenal, Manchester City na Liverpool. ***(Mail)***

### OSIMHEN KWENYE RADA

CHELSEA pia wanataka kumsajili mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, 25, ambaye ana kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa zaidi ya pauni milioni 100. ***(Sky Italia)***

### OBLAK AWINDWA MADRID

GOLIKIPA wa Atletico Madrid na Slovenia, Jan Oblak, 31, ni mchezaji mwingine ambaye yuko kwenye rada ya Chelsea msimu huu wa majira ya joto, huku klabu yake ya Hispania ikitaka kuchangisha fedha kwa ajili ya kujenga upya kikosi. ***(Fichajes)***

### TONEY AGOMBEWA LONDON

KLABU za London, West Ham United na Tottenham Hotspur, ndizo zilizo mstari wa mbele kuwania kumsajili mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney, 28, msimu huu wa majira ya joto, huku timu zote zikipanga kutoa takriban pauni milioni 50. ***(Football Transfers)***

### CASEMIRO SASA KUUZWA

KLABU ya Manchester United inajaribu kutafuta mnunuzi wa kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro, 32, msimu huu wa majiras ya joto ili kujaribu kupunguza mzigo wao wa mishahara. ***(TEAMtalk)***

### SLOT KUIBOMOA FEYENOORD

ARNE Slot, ambaye anatarajiwa kuchukua nafasi ya kocha anayeondoka Jurgen Klopp kule Liverpool, anaweza kurejea Feyenoord ili kuwasajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Mats Wieffer, 24, na mlinzi wa Uholanzi Lutsharel Geertruida, 23. ***(Football Insider)***

### MARESCA AFUATILIWA SEVILLA

KLABU ya Sevilla ni miongoni mwa timu zinazomfuatilia kocha wa Leicester City, Enzo Maresca, 44, baada ya kocha huyo kuiongoza timu hiyo kurejea Ligi Kuu England. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK: NITAKUWA SEHEMU YA MABADILIKO YA LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

NAHODHA wa Liverpool, Virgil van Dijk, amesema atakuwa sehemu ya mabadiliko ya klabu hiyo baada ya Kocha Jurgen Klopp, kuondoka kipindi cha majira ya joto.

**Klopp alithibitisha kuondoka kwake Januari, huku uvumi ukiibuka mara moja kuhusu mustakabali wa muda mrefu wa Van Dijk katika klabu hiyo.**

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, unamalizika mwishoni mwa msimu ujao, lakini amesema ananuia kuwa sehemu ya mabadiliko ya walinzi wa Liverpool, huku Kocha wa Feyenoord, Arne Slot, akitarajiwa kuteuliwa kuchukua nafasi ya Klopp.

"Kutakuwa na mabadiliko makubwa na mimi ni sehemu ya hilo," alisema Van Dijk.

**Kama nilivyosema nina furaha sana hapa, ninaipenda klabu na unaweza kuona...**

"Nadhani klabu ina shughuli nyingi na nani atakuwa kocha mpya hilo ndilo jambo kuu. Kama nilivyosema nina furaha sana hapa, ninaipenda klabu na unaweza kuona hivyo pia.

"Ni sehemu kubwa ya maisha yangu tayari, na hilo ndilo ninaweza kusema. Kutakuwa na mabadiliko mengi yatatokea na, siwezi kusema neno la kutisha ni neno sahihi, lakini ni ya kuvutia na kusisimua sana kwa kitakachotokea."

Klopp amebakiza mechi mbili kama kocha wa Liverpool, dhidi ya Aston Villa wiki ijayo, kabla ya Wolves kuzuru Anfield siku ya mwisho ya msimu.

Van Dijk, ambaye alisajiliwa na Klopp kwa pauni milioni 75 Januari 2018, alikiri kuwa itakuwa fainali ya hisia siku chache chini ya Mjerumani huyo.

"Ninajivunia kumchezea, kupigania beji na yeye na kuhesabu mafanikio tuliyopata kwa miaka mingi pia," aliongeza Van Dijk.

"Itakuwa na hisia siku ya mwisho lakini ni sehemu ya maisha wakati mwingine. Mambo mengi yanatokea nyuma ya pazia, lakini tunazingatia siku za mechi na hilo ni jukumu letu, kazi yetu na tunataka kutimiza alama sita za mwisho."

HABARI MICHEZO




# CHELSEA KUTUMIA MILIONI 97 KWA OSIMHEN

**LONDON,** England

CHELSEA imefanya mawasiliano na Napoli kuhusu uwezekano wa kubadilishana mkataba unaowahusisha washambuliaji Victor Osimhen na Romelu Lukaku, ripoti imedai.

Kumpata mshambuliaji mpya kwa muda mrefu kimekuwa kipaumbele cha kwanza kwa Chelsea katika dirisha la usajili la majira ya joto, huku Osimhen akionekana kama mgombea anayeongoza kwa sehemu kubwa ya msimu.

Mnigeria huyo alisaini mkataba mpya na Napoli mapema mwaka huu ambao una kipengele cha kutolewa chenye thamani ya zaidi ya pauni milioni 100 kwa nia ya kuwezesha kuondoka katika miezi ijayo.

Paris Saint-Germain wamemtazama Osimhen kuhusu azma yao ya kuchukua nafasi ya Kylian Mbappe, lakini Gianluca Di Marzio anadai Chelsea wamejaribu kujitosa kuwania saini yake kwa kuwasiliana na Napoli.

Chelsea wanatafuta njia za kuepuka kuzuia kipengele cha kuachiliwa cha Osimhen, ambacho kinapaswa kulipwa kwa ukamilifu, na wako tayari kutoa wachezaji wachache kwa Napoli ili kubadilishana na huduma ya Osimhen.

Katika mpango huo wanataka kumtumia Lukaku ambaye yuko kwa mkopo kule AS Roma kwa makubaliano ambayo hayajumuishi kifungu cha ununuzi. Chelsea wana makubaliano na Mbelgiji huyo kwamba atapatikana kwa ada ya pauni milioni 37 msimu huu wa majira ta joto - ikiwa ni hasara ya pauni milioni 60.5 kwa kiwango ambacho walilipa Inter mnamo 2021.

Mpango kutoka Chelsea ni kumpeleka Lukaku Napoli sambamba na ada ya kati ya pauni milioni 70, huku 'The Blues' pia wakisemekana kuwa tayari kujumuisha mchezaji chipukizi katika ofa yao ya kumleta Osimhen Stamford Bridge.

Nia ya Napoli kumnunua Lukaku, ambaye amefunga mabao 12 katika mechi 30 za Serie A akiwa na Roma msimu huu, bado haijaeleweka, ingawa mkurugenzi anayekuja wa michezo Giovanni Manna anajulikana kuwa shabiki mkubwa wa Mbelgiji huyo.

# *Mendy kupewa mkataba mpya Madrid*




**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inajiandaa kumpa beki wa kushoto Ferland Mendy mkataba mpya baada ya kufurahishwa na ubora wa Mfaransa huyo katika kipindi cha pili cha msimu, ripoti nchini Hispania zimedai.

Mkataba wa sasa wa Mendy unamalizika msimu wa majira ya joto wa 2025 na alitarajiwa kuondoka katika klabu hiyo mwaka huu baada ya kushindwa kushawishi uongozi wa Madrid kuhusu ubora wake, licha ya uungwaji mkono wa kocha Carlo Ancelotti.

Ancelotti hata alimtaja Mendy kama "beki wa kushoto bora zaidi duniani" na inaaminika amekuwa akihimiza Madrid kumpa mkataba mpya Mfaransa huyo na kwa mujibu wa Marca sasa amekubaliwa matakwa yake.

Maofisa wa Madrid wako tayari kufungua mazungumzo na Mendy kuhusu kuongeza muda, ripoti imesema, ingawa makubaliano hayafikiriwi kuwa karibu wakati huu.

Habari za mkataba mpya wa Mendy zinakuja huku kukiwa na uvumi kwamba Madrid wanapunguza nia yao ya kutaka kumnunua beki wa kushoto wa Bayern Munich, Alphonso Davies ambaye ni kama Mendy anayekaribia kumaliza miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake.

Huku wakitajwa kutaka kumfuatilia Davies msimu huu wa majira ya joto, ripoti zinasema Madrid walibadili msimamo wao na sasa wako tayari kusubiri hadi mkataba wake utakapomalizika 2025 ili kumsajili kwa uhamisho huru.

# Nunez achochea kuondoka Liverpool

**LIVERPOOL,** England

DARWIN Nunez amechochea moto uvumi wa yeye kuondoka Liverpool majira ya joto baada ya kufuta picha zote za wakati wake Anfield kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Ripoti kutoka nchini England zinasema kuwa Nunez, ambaye inasemekana anaweza kuuzwa msimu huu wa majira ya joto huku Barcelona ikiwa na nia, kwani inafuta mbadala wa muda mrefu wa Robert Lewandowski.


Baada ya tetesi hizo kuanza kuibuka, Nunez aliachwa nje ya kikosi cha kwanza Liverpool kilichoshinda mabao 4-2 dhidi ya Tottenham Hotspur, akitokea benchi kwa dakika 15 za mwisho.

Uvumi huo uliongezeka baada ya filimbi ya mwisho wakati Nunez alipoondoa kila picha inayohusiana na Liverpool kwenye Instagram yake.

Ukurasa wa Nunez bado unajumuisha picha za wakati akiwa Benfica, lakini kinachofuata ni machapisho kuhusu familia yake au Timu ya Taifa ya Uruguay.

Liverpool walilipa pauni milioni 85 kumnunua Nunez kutoka Benfica mwaka 2022 na ripoti zinaonesha tayari wamelipa jumla ya pauni milioni 76.5, huku pauni milioni 8.5 zilizosalia zikihusishwa na vipengele ambavyo havijabainishwa kuhusiana na uchezaji wa timu na mtu binafsi.

Kutokana na hali hiyo, Nunez ndiye mchezaji aliyeweka rekodi ya kusajiliwa na Liverpool, akipita pauni milioni 75 zilizolipwa kumsajili beki wa kati Virgil van Dijk, lakini mashabiki wengi wa 'Wekundu' hao wanaona hawajaona thamani ya gharama yao kubwa.



## HABARI MICHEZO

## Yanga kumfunga Aziz Ki, hofu kwa Kagera Sugar leo

INATOKA UKURASA 24

Gamondi alisema amejipanga vizuri kuhakikisha anapata pointi tatu katika mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa. Alisema anatambua ugumu wa timu hiyo, hivyo amewataka wachezaji wake kuhakikisha wanapambana ili wapate matokeo wakiwa kwenye uwanja wa nyumbani.

"Kwa upande wetu tumejiandaa vizuri kuelekea kwenye mchezo wetu wa kesho (leo) dhidi ya Kagera Sugar ni mchezo ambao utakuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa hivyo tutapambana ili tupate pointi tatu," alisema Gamondi.

Alisema kwa sasa hawazungumzii ubingwa bali anaaangalia michezo iliyopo mbele yao kwa madai kuwa iliyobaki ni migumu, jambo ambalo amewaomba mashabiki wao waendelee kuwapa ushirikiano ili washinde.

Kocha Msaidizi wa Kagera Sugar, Chacha Marwa, alisema wataingia kwa tahadhari kubwa kwa kuwa wanakutana na timu yenye ubora wa hali ya juu msimu huu.

"Mchezo utakuwa mgumu kwa kuwa Yanga ni timu ambayo ina wachezaji wenye viwango vya hali ya juu, vile vile ipo kwenye harakati za kutangaza ubingwa," alisema Marwa.

## Mgunda: Mechi na Azam ni kama fainali

INATOKA UKURASA 24

nitaisaidia Simba irudi kwenye ushindani, ninaimani wachezaji watairudisha timu sehemu nzuri, vijana waliopo wote wamepevuka na wanaelewa namna ya kufanya ili kuiweka timu katika ushindani, hivyo cha muhimu ni kuwajenga kisaikolojia na kuwarudisha kwenye morali na kila kitu kitakuwa sawa," alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Tabora United, Masoud Djuma, alisema wamecheza na timu kubwa, na mara zote wanapokuwa nyumbani huwa wanapata faida ya nyumbani.

"Tumefanya makosa na Simba wakafanikiwa kutuadhibu, tumetengeneza nafasi tumeshindwa kuzitumia. Tunasahau matokeo hayo na tunajipanga kwa mechi dhidi ya Mtibwa Sugar ili kutafuta pointi tatu, bado hatujakata tamaa tunapambana kuangalia uwezekano wa kubaki Ligi Kuu msimu ujao," alisema Masoud.

Tabora United inashika nafasi ya pili kutoka mkiani baada ya kukusanya alama 23 katika michezo 25 iliyocheza hadi sasa, huku Mtibwa Sugar ikiburuza mkia kwa pointi zake 17 zilizotokana na kushuka dimbani mara 25.

# MOROCCO AITA STARS MPYA, KUIFUATA SUDAN SAUDIA LEO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAIMU Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Hemed Suleiman 'Morocco', ametangaza kikosi cha wachezaji 21 wa timu hiyo watakaosafiri leo kulekea Saudi Arabia kucheza michezo miwili ya kirafiki dhidi ya Sudan, huku kikiundwa na idadi kubwa ya wachezaji wapya.

**Taifa Stars itacheza mchezo wao wa kwanza Mei 11 na wa pili Mei 15, mwaka huu nchini humo.**

Wachezaji walioitwa katika kikosi hichon ni Makipa; Ahmed Ali Suleiman kutoka Uhamiaji FC ya Zanzibar, Ali Salum (Simba SC) na Abrahman Vuai Nassor (U-17 TFF -TDS)

Kwa upande wa mabeki ni Mukrim Issa Abdallah (Ihefu FC), Alphonse Mabula (Msanga RFK ya Serbia), Miano Danilo (Van den Bosi - Hispania), Gadiel Michael (Cape Town-Afrika Kusini), Abdulmalik Zakaria (Namungo), Baraka Shaaban Mtui (Mashujaa FC) na Abdulrahim Seif Bausi (Uhamiaji FC - Zanzibar).

Viougo ni Mohmed Omar Sarag Boreham (Woog - Uingereza), Morice Michael Abrahaman (RFK - Serbia), Khalid Habibu Iddi (Singida FG), Ishaka Said Mwinyi (KMKM SC - Zanzibar) na Jabir Seif Mpanda (Getafe U-17, Hispania).

Washambuliaji ni Omar Abdalla Omar (Mashujaa FC), Ben Anthony Starkie (IIkeston Town-Uingereza), Oscar Adam Paul (Kakamega FC - Kenya), Kelvin Pius John (KRC Genk-Ubelgijl), Tarryan Allarakhia (Wealdstone Uingereza) na Ibrahim Hamad Ahmad (Zimamoto FC-Zanzibar).

Morocco alisema sababu za kuwaacha baadhi ya wachezaji wa muda mrefu wa timu hiyo ya taifa na kukabiliwa na katika klabu zao hususan mbio za ubingwa wa Ligi Kuu.

Aidha, alisema pia wapo baadhi ya wachezaji hawapati nafasi katika klabu zao ndio maana ni ngumu kujua uwezo wao kiuchezaji.

"Kuna utofauti mkubwa katika kikosi hichi kuanzia umri wa wachezaji baadhi yao wana umri mdogo, lakini pia wanauwezo mkubwa wa kiuchezaji, hivyo kama mwalimu nimeangalia vyote hivyo," alisema.

Hata hivyo, alisema anaamini wachezaji hao watafanya vizuri katika michezo hiyo miwili ya kirafiki nchini Saudi Arabia.

**NIMEMALIZA...**



Sarah Cyprian kutoka Barrick Runners Club, akifurahi baada ya kumaliza kushiriki mbio za Kilometa 21 (nusu marathon), za Dar City Marathon zilizofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Stumai, Aisha waingia vita ya Kiatu Ligi Kuu ya Wanawake*

**Na Saada Akida**

WAKATI Ligi Kuu ya Wanawake nchini ikibakiza raundi nne kabla ya kutamatika huku Simba Queens ikibakiza pointi nne tu kutawazwa mabingwa wapya wa msimu wa 2023/24, vita mpya ya kuwania Kiatu cha Mfungaji Bora, imeibuka.

Mastraika hatari wawili wa Kitanzania, Stumai Abdallah wa JKT Queens na Aisha Mnuka wa Simba Queens wanachuana vikali ili kutwaa Kiatu cha Dhahabu mwishoni mwa msimu wa ligi hiyo.

Licha ya kwamba timu yake inashika nafasi ya pili, Stumai wa JKT Queens anaongoza kwenye upachikaji mabao akiwa ameshacheka na nyavu mara 18, akifuatiwa na Aisha ambaye timu yake, Simba Queens inaongoza msimamo wa ligi hiyo, akiwa na mabao 16.

Aisha amesema amedhamiria kuisaidia timu yake kufikia malengo huku lengo lake la pili likiwa ni kuwa mfungaji bora msimu huu.

"Nikipata nafasi natumia kwa sababu nataka timu yangu ishinde, lakini lengo langu la pili ni kuwa mfungaji bora, mwanzoni malengo yangu yalikuwa kufunga mabao 22, lakini naona natakiwa kuzidisha ili kuwa mfungaji bora," alisema Aisha.

Katika mbio hizo za kuwania ufungaji bora Stumai na Aisha wanafutiwa kwa mbali na Winfrida Gerald ( JKT Queens) ambaye amefunga nane, Asha Djafar na Jentrix Shikangwa (Simba Queens) wakitikisa nyavu mara sita.

Donisia Minja (JKT Queens), Janeth Nyagali (Amani Queens), Hasnath Ubamba (Fountain Gate), Magreth Kunihira (Ceassia Queens) na Nelly Kache (Alliance Girls) kila mmoja amecheka na nyavu mara tano. Waliofunga mabao manne ni Amina Ramadhan (Fountain Gate), Amina Bilal na Jamila Rajabu (JKT Queens), Janeth Matulanga (Ceassia Queens), Joyce Meshack (Baobab Queens) na Kaeda Wilson (Yanga Princess).

Katika msimamo wa ligi hiyo Simba Queens wanaongoza ligi wakiwa na pointi 40 na JKT Queens ambao ni mabingwa watetezi wapo nafasi ya pili na pointi 31 ambapo kila moja inahitaji kusaka ushindi katika michezo yao iliyosalia ili kufikia malengo.

# Michezo

Jumatano Mei 8, 2024

Nipashe




Chelsea kutumia mil. 97 kwa Osimhen UKURASA 22



Aziz Ki

## Mgunda: Mechi na Azam ni kama fainali

**Na Saada Akida**

KILICHOBAKI kwa Simba ni kuwania kumaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara msimu huu, jambo ambalo Kaimu Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Juma Mgunda, amesema mechi ijayo dhidi ya Azam FC itakuwa ni kama fainali dhidi ya wapinzani wao hao.

Yanga ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 65, ikifuatiwa na Azam FC yenye alama 57 huku Simba ikishika nafasi ya tatu kwa pointi zake 53, lakini ikiwa na mchezo mmoja mkononi, hivyo kama ikishinda michezo yake yote sita iliyosalia itamaliza na pointi 71.

Kwa upande wa Azam FC ambayo itakuwa mwenyeji wa Simba kesho, ikishinda mechi zake zote tano zilizosalia itafikisha alama 72, jambo ambalo linaufanya mchezo wao huo kuwa muhimu kwa kila timu kuwania kupata matokeo chanya.

Akizungumza baada ya mechi ya Ligi Kuu kati ya timu hiyo na Tabora United juzi katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam ambao Simba ilishinda kwa mabao 2-0, Mgunda alikiri kuwa mechi ilikuwa ngumu hasa wanapocheza na timu ambazo ziko nafasi za chini zinazotaka kujinasua kushuka daraja.

"Kikubwa tumepata pointi tatu, wachezaji wangu wamepambana mechi ngumu, hatuwezi kudharau timu zilizopo chini ya msimamo. Hii mechi imeisha tunaenda kujipanga na mchezo ujao.

"Tunakutana na Azam FC, mchezo mgumu sana na tunaweza kusema ni fainali kwa sababu ndio unaotoa taswira ya kushika nafasi ya pili kwa sababu tunahitaji kumaliza kwenye nafasi hiyo," alisema Mgunda na kuongeza;

"Si rahisi, lakini naamini

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga kumfunga Aziz Ki, hofu kwa Kagera Sugar leo

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

### Gamondi atoa sababu nzito huku uongozi wa klabu hiyo ukisema tayari umefikia...

WAKATI ikielezwa kuwa katika hatua za mwisho za kumfunga nyota wake, Stephane Aziz Ki, kwa kumsainisha mkataba mpya wa miaka miwili, Kocha Mkuu wa Klabu ya Yanga, Miguel Gamondi ameihofia Kagera Sugar, akisema mechi hiyo itakayopigwa katika Uwanja wa Azam Complex, Chamanzi leo itakuwa ngumu.

Taarifa zilizolifikia Nipashe jana kutoka kwa chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, zilieleza kuwa pande zote mbili zimefikia makubaliano na kwamba kilichobaki ni Aziz Ki tu kutia saini mkataba mpya kabla ya kwenda kwao kwa mapumziko msimu huu utakapomalizika.

**Mtoa habari huyo alisema wakala wa Aziz Ki ambaye ni mama yake mzazi, alikuwapo nchini kwa ajili ya kukamilisha dili lake la kuongeza mkataba na kila kitu kimeenda vizuri baada ya mchezaji huyo kukubali kusalia ndani ya kikosi cha Yanga kwa miaka miwili mingine.**

"Mbali na Aziz Ki, kuna wachezaji wengine wapo kwenye mazungumzo ya kuongezewa mkataba akiwamo Shomari (Kibwana) ambaye Azam FC wanamhitaji. Wanaendelea kufanya mazungumzo na nyota ambao mikataba yao ipo ukingoni na wapo kwenye mipango ya Gamondi.

Kuhusu wachezaji wapya, wapo kwenye mazungumzo na Yusuph Kagoma wa Singida Fountain Gate FC, lakini wanazungumza na kiungo wa Simba, Clatous (Chama) ambaye bado mambo hayako sawa," kilisema chanzo hicho.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, amekiri kuwa baadhi ya nyota wao mikataba yao ipo ukingoni na wako nao katika mazungumzo akiwamo Aziz Ki na nyota wengine ambao wapo kwenye mipango ya kocha Miguel kwa msimu ujao.

"Mkataba wa Aziz Ki unafikia ukingoni na utamalizika mwishoni mwa msimu huu, ninachokijua sasa hawezi kujiunga na timu nyingine, moja ya mikakati ya Rais wa Yanga, Hersi (Saidi) ni kuhakikisha wachezaji wetu bora wanasaini mkataba mpya akiwamo Stephane," alisema Kamwe.

Wakati huo huo, kuelekea mchezo wao wa leo dhidi ya Kagera Sugar, Gamondi aliiambia Nipashe kuwa mechi hiyo itakuwa ngumu kutokana na ubora wa wapinzani wao hasa akikumbuka mechi ya kwanza ugenini walitoka sare.

Yanga inashuka dimbani ikitoka kuvuna pointi tatu katika Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma dhidi ya Mashujaa FC, huku Kagera Sugar ikitoka kuambulia alama moja dhidi ya KMC kutokana sare ya kutokufungana.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >